Jumanne Mei 12, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580229

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Mpaka Tanzania na Zambia wafungwa madai ya corona

UKURASA 3


Nipashe

TESA

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Baada ya corona kutisha kambi za taaluma mkoa waibuka kivingine

SAYANSI

NA GAUDENSIA MNGUMI

Simu za mikononi kitisho kingine uhai, mazingira

UKURASA 11

# Chadema yatimua wabunge 4 wakaidi

**MMOJA** avuliwa nyadhifa, 11 watakiwa kujieleza, Ndugai awatetea... *Endelea ukurasa 2*



Geti la kuingia nchini Zambia, kupitia mpaka wa Tunduma, mkoani Songwe, likiwa limefungwa upande wa nchi hiyo, jana, baada ya serikali ya nchi hiyo, kufunga mpaka wake na kusitisha shughuli zote za forodha. **PICHA: MANUEL KAMINYOGE**

# Sukari kizungumkuti, serikali kutoa tamko leo

UKURASA 2

## AWEKA WATOTO REHANI KUKOMBOA NG'OMBE WAKE

UKURASA 4

## BAA LA CORONA



Katika kujiweka fiti kipindi hiki cha janga la corona, usikimbilie kufanya mazoezi ya muda mrefu kama haujazoea. Anza taratibu kwa dakika tano hadi 10, kidogo kidogo kwa kuongeza mpaka dakika 30 kadiri siku zinavyoongezeka. WHO

* **Epuka mikusanyiko ya watu**
* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**


Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

**MICHEZO** UKWELI MWAMNYETO USAJILI SIMBA, YANGA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA



Wafanyabiashara wadogo na wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma, wakiwa kwenye foleni ya kusubiri kupata sukari katika duka la kampuni ya Mohamed Enterprises, kutokana na bidhaa hiyo kuadimika. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

# Upatikanaji sukari wawa kizungumkuti

**Na Waandishi Wetu**

UPATIKANAJI wa sukari nchini umezidi kuwa tete, hivyo watu kupanga foleni ili kupata kiasi kidogo, huku nyingine ikipatikana kwa bei ya juu hadi Sh. 5,000 kwa kilo moja.

Katika baadhi ya maeneo wananchi wameonekana wakihahaha kuisaka, na wengine kuamua kutumia miwa na asali badala ya bidhaa hiyo.

Mkoani Morogoro na Ruvuma, wananchi walionekana wakiwa kwenye misururu mirefu katika maduka, huku jijini Tanga, ikikosekana na Dar es Salaam kupatikana baadhi ya maeneo kwa bei tofauti.

Wilayani Kinondoni, Mkuu wa wilaya hiyo, Daniel Chongolo, aliieleza Nipashe kuwa wafanyabiashara wameficha bidhaa hiyo, na kwamba serikali inashughulikia kuhakikisha inapatikana.

Aidha, Mbunge wa Mahenge, Goodluck Mlinga, alipeleka hoja bungeni na ilijibiwa na Spika kuwa leo serikali itatoa taarifa rasmi bungeni.

**DAR YAADIMIKA**

Jijini Dar es Salaam robo kilo ya sukari inauzwa Sh. 2,000 kwa watu wachache wanaofahamiana na muuzaji, huku wengine wakificha kabisa.

Nipashe ilitembelea maeneo ya Kinondoni na Sinza ambao walisema hawana, lakini wanapoona mtu anaondoka wanamuita na kumuulizia kama atakuwa tayari kununua kwa Sh. 4,000 kwa kilo moja.

Baadhi ya wafanyabiashara wa rejareja walisema wanaopaswa kukamatwa na kuchukuliwa hatua ni wauzaji wa jumla kwa kuwa huwauzia mfuko wa kilo 100 kwa Sh. 145,000 ikiwa ni sawa na kununua kilo moja Sh. 2,800 huku bei elekezi ya sukari ikiwa ni Sh. 2,600.

**DC AWATULIZA WANANCHI**

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Chongolo, amewatoa hofu wananchi kuhusu suala la sukari wilayani humo na kuahidi usambazaji utarejea hivyo wasikimbilie kununua nyingi isiyo na mahitaji kwa wakati huu.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam, Chongolo alisema sukari ipo nyingi na ikifika kwenye maduka wananchi wanunue kulingana na mahitaji waliyonayo.

"Ninatoa pole wananchi wa wilaya yangu kwa usumbufu uliojitokeza kuhusu tatizo la upatikanaji wa sukari kutokana na ukaidi wa baadhi ya wafanyabiashara kwenye suala la utekelezaji wa bei elekezi ya Sh. 2,600 iliyotolewa kwa mkoa wa Dar es Salaam," alisema.

"Sukari ipo lakini wafanyabiashara hawataki kuiingiza kwenye mzunguko, uamuzi wa serikali wa kupanga bei elekezi ulisukumwa na uwepo wa shehena ya kutosha ya sukari inayozalishwa ndani na inayoagizwa kutoka nje ya nchi," alisema.

**TANGA BEI YA CHAI YAPANDA**

Jijini Tanga bei ya chai ya rangi na maziwa imepanda kutoa Sh. 300 hadi 500 na 1,000 wenye migahawa na mahoteli, huku wananchi wakitumia miwa kama mbadala wa sukari kwenye chai.

Nipashe lilitembelea migahawa na mahoteli na kukuta mabango yenye maelekezo yakupanda kwa bei ya chai ambapo migahawa iliyokuwa ikiuza kikombe cha chai ya rangi kwa Sh. 100 sasa kinauzwa kati ya Sh. 300 na Sh. 500, huku chai ya maziwa awali ilikuwa inauzwa Sh. 500 sasa ni Sh. 800 hadi Sh. 1,000 huku kwenye mahoteli chai ya rangi inauzwa Sh. 1,000 na 1,500.

Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Thobias Mwilapwa, akizungumza na madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Tanga wiki iliyopita, alisema walifanya msako maalumu kwa wafanyabiashara wa sukari wanaouza bei ya juu na kuwakamata sita.

Ofisa Biashara wa Wilaya ya Pangani , Mohamed Hussein, aliwaonya wafanyabiashara kutotumia mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kuwapandishia wananchi bei.

**DODOMA YAZIDI KUPAA**

Jijini Dodoma kilo moja ya sukari inauzwa Sh. 4,000 kwa kilo moja katika maeneo mengi, huku ikiadimika kabisa kwingine.

Akizungumza na Nipashe mmoja wa wakazi wa Jiji la Dodoma Mtaa wa Makole, Amina Salum, alisema: "Hivi sasa ukiibahatisha sukari bei angalau ya chini ni Sh. 4,000, lakini katika maduka mengi hakuna kabisa sukari, hivyo tunapata tabu sana na wakati huu wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani."

**SIMIYU YAFIKIA 4,000**

Mkoani Simiyu katika maeneo mengi inauzwa kati ya Sh. 3,000, 3,500 hadi 4,000, licha ya jitihada za kufanya msako, huku kingine ikiuzwa kwa siri.

**ZANZIBAR BEI POA**

Visiwani Zanzibar sukari inauzwa kwa Sh. 1,800 bila kuwapo uhaba.

**SPIKA: SERIKALI KUTOA KAULI LEO**

Spika wa Bunge, Job Ndugai, amesema leo serikali italitolea ufafanuzi suala la uhaba wa sukari unaondelea nchini, amewataka wabunge kuwa na subira.

Alisema Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, atalitolea ufafanuzi suala la uhaba wa sukari. Spika Ndugai alilazimika kutoa ufafanuzi huo baada ya Mbunge wa Ulanga, Goodluck Mlinga kuomba mwongozo wa Spika kuhusu uhaba wa sukari nchini.

Mlinga alisema: " Hadi sasa bunge halijapata taarifa yoyote kuhusu uhaba wa sukari unaendelea sasa nchini, wananchi wanapata tabu, wanahangaika, sasa naomba kiti chako kitoe ufafanuzi wa suala hili".

Wiki iliyopita akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, alilieleza bunge kuwa zimeangizwa tani 40,000 za sukari na zimechelewa kufika kutokana na janga la corona kwa kuwa meli ya kuleta shehema ilikosekana.

***Imeandikwa na Romana Mallya (DAR), Boniface Gideon (TANGA), Gwamaka Alipipi na Paul Mabeja (DODOMA), Happy Severine (SIMIYU) na Rahma Suleiman (ZNZ)***

# Chadema yatimua wabunge 4 wakaidi

**Na Waandishi wetu**

SIKU 12 baada ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo(Chadema), kuwataka wabunge wake wasihudhurie vikao vya Bunge na kujiweka eneo la kujitenga kwa siku 14, jana kimewafukuza uanachama wabunge wanne, huku 11 wakitakiwa kujieleza kwanini wasichukuliwe hatua za kinidhamu.

Aidha, chama hicho kimemvua nyadhifa zote za Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama hicho, Mariam Msabaha, ambaye pia ametakiwa kujieleza kwa nini asichukuliwe hatua zaidi, na kwamba alipaswa kuwa mstari wa mbele kutekeleza maazimio hayo.

Wabunge waliofukuzwa ni Antony Komu (Moshi Vijijini), Joseph Selasini (Rombo), Wilfred Rwakatare (Bukoba Mjini) na David Silinde(Mbozi).

Kabla ya kufukuzwa, Silinde alitakiwa kujiuzulu nafasi zake zote ikiwamo Katibu wa Wabunge wa Chadema na Waziri Kivuli wa Viwanda na Biashara.

Selasini alilalamika kuondolewa kwenye kundi songezi la wabunge wa Chadema, hivyo kushindwa kupata nafasi ya kuchangia mjadala wowote bungeni hadi alipopitisha ombi lake kwenye meza ya Spika.

Waliotakiwa kujieleza wabunge wa Viti Maalum Suzan Masele, Joyce Sokombi, Rose Kamili, Latifa Chande, Lucy Mlowe, Sware Semesi, Sabrina Sungura na Anne Gideria.

Wamo pia Mbunge wa Moshi Mjini, Jaffary Michael, Mbunge wa Kilombero, Peter Lijualikali na Mbunge wa Karatu, William Kambalo.

Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika, alitangaza uamuzi huo jana kwa njia ya mtandao na kueleza kuwa hatua hiyo imefikiwa baada ya uamuzi wa kikao cha Kamati Kuu.

Mnyika alisema Kamati Kuu baada ya kutathmini utekelezaji wa msimamo, makubaliano na maagizo ya chama kiliyoyafanya na wabunge wake kuhusu kujitenga kwa siku 14 na kubaini baadhi kuyakiuka, kiliamua kuchukua hatua hizo.

Alisema uamuzi huo ni kwa mujibu wa Katiba, taratibu na muongozo wa chama hicho.

"Na chama kilifanya hivi kwa kuzingatia umuhimu wa Katiba na miongozo ya chama chama kinao muongozo wa kusimamia wabunge, halmashauri, madiwani na viongozi wengine wanaotokana na tiketi ya Chadema," alisema Mnyika.

Aliongeza: "Na muongozo huu ipo sehemu mahususi inayohusu wabunge wa Chadema. Katika kifungu cha pili na kipengele A cha muongozo wa chama, kimeeleza kwamba mbunge anatakiwa kutii na kutimiza maagizo anayopewa na chama kupitia vikao halali, na kama hakubaliani na maagizo hayo, aeleze hivyo kupitia taratibu na ngazi zilizowekwa na Katiba ya chama."

"Na kwa muongozo huu, vile vile kipengele B kinasema kutakuwa ni mwiko kwa Mbunge kukashifu chama au kiongozi wa chama, ndani au nje ya Bunge."

Kwa mujibu wa Mnyika, Komu na Selasini pamoja na kwamba wamejipotezea sifa ya uanachama kwa kujitangazia kwamba hawakubaliani na itikadi ya Chadema, lakini wameendelea kutoa kauli za kejeli, kashfa na kukiuka maagizo ya chama na kwa sababu hizo.

Mnyika alisema Kamati Kuu imemuelekeza Katibu Mkuu kumuandikia barua Spika wa Bunge juu ya uamuzi huo.

Kuhusu Rwakatare na Silinde, Mnyika alisema nao siyo tu wamekiuka maagizo ya chama hicho, bali pia nao wameku wakijitokeza kwenye vyombo vya habari na njia nyingine za mawasiliano kutoa maneno ya kashfa na kejeli dhidi ya maagizo na chama na viongozi wake.

Alisema wabunge wengine 11 wamepewa nafasi hiyo ya kujieleza kwa sababu pamoja na kwenda kinyume cha maagizo ya chama hicho, lakini hawakuonyesha utovu wa nidhamu kwa kukikashfu, kukejeli au kutoa maneno yasiyofaa kwa chama na viongozi wake.

Aidha, chama kimewataka wabunge kuendela kujitenga kwa siku 14 na zikiisha na kuona wako salama warejee bungeni.

**WAENDELEA KUINGIA BUNGENI**

Licha ya wabunge hao kutangaziwa uamuzi wa chama chao, jana baadhi walionekana bungeni na walichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**SPIKA KUWALINDA**

Spika wa Bunge, Job Ndugai, amewataka wabunge waliofukuzwa waendelee kuhudhuria vikao vya bunge kama kawaida, na kwamba hatambui uamuzi uliotolewa.

Pia amemwagiza Msajili wa Vyama vya Siasa kuviangalia baadhi ya vyama ambavyo vinaendesha shughuli zake kiubabe. "Wabunge wanaapishwa na Spika, msiwe na wasiwasi, hivyo ni vikao vya majungu vilivyowafukuza, eti mtu mmoja ana uamuzi wa kufanya vile atakavyo, ataishia huko huko, lakini siyo Tanzania, wananchi wamechagua mbunge halafu huyo mbunge eti anakwenda kuwa mtumwa wa mtu, hicho kitu hakikubaliki," alisema Ndugai.

Aidha, alisema leo atatoa orodha ya wabunge ambao hawajatii masharti ya kiti ya kurudi bungeni wakiwa wamepimwa virusi vya corona

Wabunge waliofukuzwa walisema wanashangazwa na hatua hiyo kwa kuwa hatua dhidi yao imechukuliwa bila wao kushirikishwa.

***Imeandikwa: Elizabeth Zaya (DAR) na Gwamaka Alipipi (DODOMA)***

## HABARI KITAIFA

# Tunduma walia Zambia kufunga mpaka

**Na Manuel kaminyoge, SONGWE**

MAMIA ya wafanyabiashara wa mji wa Tunduma, Wilaya ya Momba, mkoani Songwe, wameiangukia serikali kufuatia nchi ya Zambia kufunga mpaka wake na shughuli zote za forodha kusimama.

Mpaka wa Tanzania na Zambia unategemewa na nchi za Jumuiya ya Ushirikiano wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na hatua hiyo inaweza kuleta madhara makubwa kwa nchi zote zinazotegemea mpaka huo.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jeneral Nicodemas Mwangela, amewataka wafanyabiashara wote raia wa Tanzania wenye maduka upande wa Zambia kufuata sheria zilizowekwa na nchi hiyo.

Mwangela alisema wafanyabiashara wanatakiwa kufuata sheria za Zambia kama walivyozifuata wakati wa kuweka maduka upande huo.

Vile vile, katika hatua nyingine mkuu huyo amewataka wafanyabiashara kuendelea na shughuli za kiuchumi katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma ambao uko katika mpaka wa Tanzania na Zambia ikiwa tayari nchi ya Zambia imefunga mpaka wake wa Nakonde kuanzia jana Mei 11, 2020.

Akizungumza na wananchi katika eneo la Tunduma jana, Mwangela alisema Tanzania haijafunga mpaka wala kufunga shughuli zozote za kiuchumi hivyo wananchi wa eneo hilo waendelee kufanya shughuli za kiuchumi na kibiashara.

"Sisi hatujaweka lockdown, tuendelee na shughuli zetu, wananchi wa Tunduma mko huru chapeni kazi ila tufuate maagizo ya serikali ya kujikinga na corona kwa kuvaa barakoa, kuepuka mikusanyiko na kunawa kwa maji tiririka na sabuni, tufanye kazi huku tunajilinda na corona," alisema.

Pia, aliwataka wananchi wa Tunduma na Mkoa wa Songwe kufuata maelekezo yaliyotolewa na Zambia ya kutovuka mpaka kufanya biashara bali kwa sasa biashara ziendelee upande wa Tanzania hadi hapo mpaka utakapo funguliwa.

John Mtafya, mkazi wa Tunduma aliipongeza Serikali ya Tanzania kwa kuruhusu shughuli za kiuchumi kuendelea katika mpaka wa Tunduma licha ya kuwa kufungwa kwa upande wa Zambia kutaathiri uhusiano wa kibiashara kati ya nchi hizo mbili.

Mtafya alisema wafanyabiashara wa Tunduma wataendelea na biashara kama ilivyokuwa awali huku wakijilinda dhidi ya ugonjwa wa corona kama serikali ilivyoelekeza.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tunduma, Regina Bieda, aliwataka wafanyabiashara kujifunza na kuacha tabia ya kwenda kujenga maduka upande wa Zambia badala yake waende kwenye maeneo yaliyotengwa na nchi ya Tanzania.

Alisema maeneo ya upande wa Tanzania hayajaisha hivyo haina haja Watanzania kwenda kuweka maduka upande wa Zambia.

Akizungumza kwa niaba ya Rais wa Zambia, Edgar Chagwa Lungu, jana, Waziri wa Afya wa nchi hiyo, Chitalu Chilufya, alitangaza uamuzi wa kufunga mpaka kufuatia ripoti ya wagonjwa 76 wa corona katika mji wa Nakonde mpakani mwa Tanzania na Zambia.

## BoT yakamata sarafu za mil. 200/- zikichezwa kamari

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), jana imekabidhiwa sarafu za Sh. 200 na 500 zenye thamani ya Sh. milioni 200 na Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Regina Chonjo, zilizokuwa zikichezeshwa kamari na kuhifadhiwa nyumbani kinyume na sheria.

Akipokea fedha hizo, Mkurugenzi wa tawi la BoT, Kanda ya Kati Dodoma, Richard Wambali, amewataka wananchi kuacha kutumia fedha kwa matumizi yasiyo sahihi ikiwamo kucheza michezo ya kubahatisha kwa kuwa ni kosa kisheria.

Alisema kuwa kitendo cha baadhi ya wananchi kutumia fedha za Tanzania katika matumizi yasiyosahihi kunaweza kusababisha kushusha thamani ya fedha na kutoa rai kwa jamii kufichua watu wanaofanya hivyo ili kulinda thamani ya pesa.

"Ipo haja kwa wadau kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi sahihi ya fedha za Tanzania kwa sababu tulichokikuta hapa ni kitendo cha kihalifu na kinashusha thamani ya pesa yetu," alisema Wambali.

Alisema, inasikisha kuona kuwa wakati wananchi wanahangaika uhaba wa chenji mitaani, baadhi ya watu wamezihifadhi ndani kinyume na sheria za nchi.

Kaimu Meneja huduma za kibenki katika kanda hiyo, Nolasko Maluli, alisema kampuni hiyo ya Bonanza imefanya kosa la kutumia fedha kuchezea badala ya tokeni zao.

Alieleza kuwa baada ya kufanya ukaguzi katika mashine zilizokuwa zikichezesha mchezo huo wa kubahatisha, walikuta sarafu za 200 kinyume na sheria za Benki Kuu ambayo ndio inayohusika na utengenezaji na usimamizi wa matumizi ya fedha.

"Tumebaini kwenye hizi mashine zao wanatumia hizi fedha kuchezea na zinapozungushwa kwenye mitambo yao zinachakaa na nyingine zinaharibika kabisa sasa huu ni ukiukaji wa sheria," alisema Maluli.

Alisema mashine zaidi ya 20 zimewekewa vipuri vya sarafu hizo jambo ambalo ni kinyume na taratibu za matumizi ya fedha.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA**
**TASAC**

# TANZIA



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), kwa masikitiko makubwa anatangaza kifo cha Mkurugenzi wa Ulinzi, Usalama wa Vyombo vya Usafiri Majini na Utunzaji wa Mazingira ya Bahari (DMSE) **Mhandisi Japhet L. Loisimaye** kilichotokea tarehe **10 Mei, 2020 jijini Dar es salaam.**

Mkurugenzi Mkuu anatoa pole kwa Familia, Wafanyakazi na wote walioguswa na msiba huu.

Hakika atakumbukwa kwa **Uchapakazi, Uadilifu na Uzalendo katika kipindi chake chote cha uhai wake.**

Tunawaombea wote faraja na subira njema katika kipindi hiki kigumu cha majonzi.
Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.

AMIN
**Imetolewa na;**

**MKURUGENZI MKUU**
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA (TASAC).**

# Aweka watoto rehani kukomboa ng'ombe wake

**Na Romana Mallya**

Mfugaji Lenina Saturo, amesimulia huku akitokwa na machozi namna ambavyo alilazimika kuwaweka watoto wake wa kike rehani ili aendeshe kesi ya kugomboa ng'ombe wake 311.

Saturo alisimulia kuwa baada ya mifugo yake kukamatwa kwa madai kuwa imeingia hifadhi ya ...kesi ilipelekwa mahakamani.

Alisema baada ya hukumu kutoka Oktoba 3, mwaka 2018 hadi sasa hajapata mifugo yake na kujikuta akibaki peke yake baada ya wake zake kurudi kwao na watoto wakiwa rehani.

Saturo alisimulia kuwa akiwa hospitalini akiuguza majeraha baada ya ajali aliyoipata, huku nyuma ng'ombe zake 311 zilikamatwa.

"Wadogo zangu na watoto waliokuwa nyumbani siku hiyo ndiyo waliosaidia, kwa sababu nilikuwa hospitali, baada ya ng'ombe kukosekana siku moja ndipo wakasema zimeibiwa na baadaye zilikutwa katika Wilaya ya Kondoa na kusema zimekamatwa kwenye hifadhi," alisema.

Alisema vijana waliokuwa wakifuatilia mifugo hiyo nao walikamatwa kwa madai kuwa walichunga kwenye hifadhi.

"Baada ya kufuatiliwa Kondoa ikabainika hazikuingia kwenye hifadhi au kama ziliingia kule ni mbali, Mahakama ya Wilaya ya Kondoa iliamuru ziachiliwe na vijana waachiwe.

"Meneja alikata rufani kuja Dodoma na hukumu ilitoka Oktoba 3, mwaka 2018 mpaka leo sijapata mifugo yangu, nilipofuatilia mahakamani, waliitwa Mwendesha Mashtaka atoe vielelezi vya kuachia ng'ombe na hakuja.

Alisema waliitwa na Mbunge wa Kiteto, ambaye aliwataka wakachukue ng'ombe wao.

"Tukaambiwa kwamba ng'ombe wamekwenda kuhesabiwa na kati ya ng'ombe 311 walibaki 197, nina wake sita na watoto 43," alisema.

Saturo alisema alijaribu kufuatilia kesi hiyo, lakini imeshindikiana kwa sababu hana nguvu hajabaki na chochote.

Ali sema watoto amewapeleka kwa ndugu zake na wake zake wametoroka kwenda kwao na mifugo yake hajaipata hadi sasa.

"Nikashindwa sina nguvu tena kwa sababu fedha niliyokuwa ninaendeshea kesi ilikuwa na riba nikawa nauza watoto," alisema.

Saturo akisimulia huku akitokwa na machozi, alisema alikuwa akiuza watoto wake wadogo ili alipe riba na hajafanikiwa kupata ng'ombe. "Ninapenda kuonana na Rais (John Magufuli), kwa sababu ninajua ni mtetezi wa wanyonge ninajua anajua walemavu na watoto yatima anawajua, ninamuomba kwa sababu huku hakuna haki.

"Niliposhinda kesi nilijua ni chombo cha haki, ninapenda kumuona Rais kama sijamuona ni bora ninywe sumu kwa sababu sina nguvu tena, ninajua Rais ni baba yetu tunamtegemea anajua wafugaji na watu wenye walemavu na wanyonge. Kama atanisaidia ili nipate hata kidogo ili nikawakusanye watoto wangu."

Wakati Saturo akieleza hayo, Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), kimeeleza ukiukwaji wa sheria na uonevu unaofanywa na mamlaka za hifadhi dhidi ya mifugo ambapo hadi sasa iliyotaifishwa ni 1,955 na iliyouawa ni zaidi 5,000.

Kupitia tamko lao walilolitoa jana kwa pamoja na kusainiwa na Mwenyekiti wa CCWT, George Bajuta na Katibu Mkuu Magembe Makoye, wafugaji wamekuwa wakikabiliwa na changamoto hizo.

"Kumekuwa na utaifishaji wa mifugo usiozingatia sheria katika hifadhi mbalimbali za misitu na za wanyamapori ambao umesababisha umaskini na mateso kwa wafugaji," walisema.

Viongozi hao walisema kuwa utaifishaji huo umefanyika maeneo mbalimbali nchini licha ya baadhi ya kesi zikiwa mahakamani na nyingine wafugaji wakiwa wameshinda.



Mafundi waliopewa kandarasi ya ujenzi wa daraja linalounganisha Kata Kisiwani/Msindo, Wilayani Same, mkoani Kilimanjaro, wakiendelea na kazi ya kilijenga daraja hilo lililosombwa na maji jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Bil. 600/- kulipa madeni ya watumishi

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 600 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa ya watumishi wa umma kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ikiwa ni moja ya mkakati wa kuleta nidhamu na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alisema hayo alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Bumbwini, Muhammed Amour Muhammed, aliyetaka kujua ni lini serikali italipa madeni ya watumishi wa umma kutokana na madeni hayo kuongezeka.

Dk. Kijaji alisema serikali imetenga Sh. bilioni 600 ambazo zimeidhinishwa na Bunge ili kugharamia malipo ya madeni mbalimbali ikijumuisha madeni ya watumishi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

"Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya Sh. bilioni 364.7 zimelipwa kama madai ya watumishi, wazabuni na makandarasi na kati ya hizo Sh. bilioni 97.6 zimelipwa kama madeni ya watumishi pekee," alisema Dt. Kijaji.

Alisema katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 hadi 2019/2020 jumla ya Sh. bilioni 375.7 zilitolewa kugharamia madeni mbalimbali, kati ya fedha hizo Sh. bilioni 113.8 zilitumika kulipa madeni ya mshahara na Sh. bilioni 261.9 madeni yasiyo ya mshahara.

Alifafanua kuwa, kutokana na changamoto ya uwapo wa madeni hewa, serikali ilizuia ulipaji wa madeni kabla ya kuhakikiwa lengo likiwa ni kuleta nidhamu ya matumizi ya fedha za umma.

Vile vile, alisema kutokana na takwimu hizo, serikali inajisikia fahari na inahitaji kupongezwa kutokana na juhudi mbalimbali inazochukua kuhakikisha madeni yote ya watumishi yanalipwa kwa wakati ikithibitika yana uhalali.

*Imeandikwa na Farida Ramadhani na Peter Haule, WFM, Dodoma

# Kesi mauaji Dk. Mvungi yahamishiwa Korti Kuu

**Na Hellen Mwango**

HATIMAYE kesi ya mauaji ya aliyekuwa Mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Dk. Sengondo Mvungi, imehamishiwa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kwa mara ya pili baada ya washtakiwa sita kusomewa maelezo ya mashahidi.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni, Msigwa Matonya, Mianda Mlewa, Paulo Mdonondo, Juma Kangungu, Longishu Losingo na John Mayunga.

Upande wa Jamhuri jana uliwasomea maelezo ya mashahidi mbele Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Aprili, 6, 2017 washtakiwa hao walisomewa maelezo ya mashahidi kwa mara ya kwanza na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Patrick Mwita, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Jana, Wakili wa Serikali, Anna Chimpaye, alidai kuwa upande wa Jamhuri unatarajia kuita mashahidi 33 na vielelezo 18, kesi hiyo itakapoanza kusikilizwa Mahakama Kuu.

Chimpaye alitaja vielelezo hivyo kuwa ni cheti cha kifo, ripoti kutoka kwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na ramani ya tukio.

Pia, katika mashahidi watakaotoa ushahidi mahakamani hapo ni pamoja na Mjumbe Ally Abdalah wa shina namba 33 eneo la Kiwalani Migombani, jijini Dar es Salaam.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa Novemba 12, 2013 Mjumbe huyo akiwa nyumbani kwake walifika watu watano wakitaka kufanya upekuzi katika nyumba ya Mayunga maarufu kama Ngosha.

Katika upekuzi huo walikuta bastola ndogo aina ya Revolva, risasi 21 na baruti nne zilizokuwa ndani ya mfuko wa nailoni zilizofichwa ndani ya nyumba hiyo juu ya paa la nyumba pembeni.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na shtaka la mauaji kwa kudaiwa kuwa Novemba 3, mwaka 2013, walifanya kosa la mauaji ya kukusudia kinyume na kifungu cha 196 cha sheria na kanuni ya adhabu sura ya 16, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Ilidaiwa kuwa siku hiyo ya tukio, katika eneo la Msakuzi Kiswegere, Wilaya ya Kinondoni, washtakiwa hao kwa pamoja walimuua kwa kukusudia Dk. Mvungi.

# Serikali kuangalia mianya kunusuru sekta utalii

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

SERIKALI imesema sekta ya utalii imeathirika zaidi na janga la ugonjwa wa corona, hali inayolazimisha wao na wadau wakutane Arusha kuangalia mianya ya kufungua sekta hiyo kwa ajili ya kuinusuru.

Akizungumza jana jijini hapa, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kingwangalla, wakati alipokuwa na wadau wa sekta ya utalii nchini, alisema wamekutana ili kufanya maandalizi ya mpango wa kupokea watalii baada ya janga la Covid -19.

"Janga hili litakapoisha tunatamani, sekta ya utalii iwe ya kwanza kuamka na sasa kuna utafiti mbalimbali unaoendelea ili kuinusuru sekta hii, maana ni nyeti inayoingizia fedha nyingi za kigeni nchi yetu," alisema.

Alisema ni vyema sasa wajadiliane jinsi ya kuweka mambo mbalimbali ili kuifungua sekta ya utalii, ingawa si jambo rahisi maana imeathirika na ugonjwa huo kwa sehemu kubwa, hivyo lazima wajadili na kuweka mikakati ya mbele kabla ya kufungua milango ya kibiashara.

"Tuna kila sababu ya kujenga imani katika soko hili la utalii ikiwamo upimaji wa corona kwa wageni wetu na jinsi ya kudhibiti, sababu hatutaki tumwambukize virusi mtalii na sisi tusiambukizane," alisema.

Kigwangalla alisema ni lazima waangalie misingi ya afya iliyotolewa na inayotolewa na sekta hiyo, wakati wakishuhudia nchi mbalimbali zikianza kufungua mipaka yake na wao wakijipanga kutekeleza viwango vinavyotakiwa ili waweze kuhudumia watalii watakaokutwa na virusi wanapofika nchini.

"Nasisitiza ugonjwa huo upo, hivyo ni lazima sasa tutafute mbinu za tahadhari kudhibiti ugonjwa huo tunazichukuwa ikiwamo kuhakikisha tunajaribu kufanya utalii kwa tahadhari kubwa na kuzingatia maelekezo yote yanayotolewa na wizara husika," alisema.

Alisema masuala yatakayojadiliwa katika mkutano huo, lazima waweke imani na kufuata muongozo unaokubaliwa na serikali, ikiwamo kuweka viwango vinavyotakiwa.

"Leo Nitaongea kwa kina na vyombo vya habari, ili kusema yale tuliyokubaliana," alisema.

Alisisitiza kuwa sekta hiyo imeathirika sana hasa kwa familia zinazotegemea sekta ya utalii, sekta binafsi, sekta ya hoteli, hivyo lazima wajadiliane na watakayokubaliana watayafikisha katika mamlaka zinazohusika.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda, alisema kikao hicho ni muhimu na ni lazima watu wawe wazalendo kuhakikisha sekta ya utalii inanyanyuka tena.

Kikao hicho kinashirikisha washiriki kutoka Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa), Mamlaka ya Hifadhi ya Njiro (NCAA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Tawa), Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), pamoja na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Uhamiaji.



Mgambo wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, akimpima joto Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, kabla ya kuhutubia Baraza la Madiwani kupitia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za mwaka 2018/19, mwishoni mwa wiki. **PICHA: TIGANYA VINCENT**

# Ukusanyaji madhuhuri sekta ya ardhi wapaa

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Willium Lukuvi, amesema katika kipindi cha miaka mitano, makusanyo na maduhuli yatokanayo na sekta ya ardhi yameongezeka kutoka Sh. bilioni 74.71 mwaka 2015/16 hadi Sh. bilioni 100 kwa mwaka 2019/20.

Alisema ongezeko hilo limechangiwa na hatua za makusudi zilizochukuliwa na wizara ikiwamo kuimarisha matumizi ya mifumo ya ukusanyaji mapato kwa njia ya kielektroniki na kuongezeka kwa idadi ya walipa kodi.

Alisema katika kutekeleza azma ya kuboresha mfumo wa utoaji haki nchini, ikiwa ni pamoja na utatuzi wa migogoro ya ardhi, kuanzia mwaka wa fedha 2020/21, Serikali inakusudia kuhamishia shughuli za mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya katika mhimili wa Mahakama.

Aliyasema hayo jana bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2020/21, na kuomba kuidhinishiwa Sh. bilioni 133.568.

"Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa kwa kipindi cha miaka mitano, hali ya makusanyo ya maduhuli yatokanayo na sekta ya ardhi imeendelea kuimarika. Makusanyo haya yameongezeka kutoka Sh. bilioni 74.71 mwaka 2015/16 hadi kufikia wastani wa Sh. bilioni 100 mwaka 2019/20," alisema na kuongeza:

"Ongezeko hili limechangiwa na hatua za makusudi zilizochukuliwa na wizara ikiwamo kuimarisha matumizi ya mifumo ya ukusanyaji mapato kwa njia ya kielektroniki na kuongezeka kwa idadi ya walipa kodi."

Alisema wizara inaendelea kuweka utaratibu wa namna ya kuhakikisha kila mmiliki wa ardhi anachangia pato la taifa kupitia kodi, tozo na ada mbalimbali zinazotokana na sekta ya ardhi.

Aidha, Waziri Lukuvi alisema kwa kipindi cha miaka mitano, wizara yake imekuwa na mikakati ya mbalimbali ya kushughulikia utatuzi wa migogoro.

Alisema jumla ya migogoro 15,808 ilitatuliwa kwa njia ya kiutawala katika halmashauri mbalimbali nchini , migogoro 131,603 ya matumizi ya ardhi ilitatuliwa kupitia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

Waziri Lukuvi alisema katika kuunga mkono dhana ya Tanzania ya viwanda jumla ya ekari 284,349.07 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda katika miji mbalimbali nchini iliyoandaliwa.

Alisema wizara kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji itaendelea kufuatilia utekelezaji wa mipango kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na miongozo iliyopo.

Hivyo, alizitaka mamlaka za upangaji kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya uandaaji, utekelezaji wake na kudhibiti uendelezaji miji ili uendane na mipango iliyopangwa.

## UFUPI

### 'Benki ya Kilimo ipunguze riba'

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SERIKALI imeagiza Benki ya Kilimo nchini kuhakikisha inashusha riba kutoka asilimia 11 hadi 9 kwa mkulima wa kahawa kupitia vyama vya Chama Kikuu cha ushirika Kagera(KCU) na Chama Kikuu cha Ushirika Karagwe na Kyerwa(KDCU).

Aidha, imesema haizuii sekta binafsi kununua kahawa isipokuwa imewakataza kununua kwa mkulima moja kwa moja.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alipokuwa akizungumza na viongozi kutoka mikoa inayolima zao la Kahawa hapa nchini.

Bashe alisema lengo la kuitaka benki hiyo ishushe riba ni kuwasaidia wakulima kuendesha kilimo hicho.

Alisema wakulima hao wamekuwa wakipata hasara kwenye kilimo hicho, hivyo serikali inataka wanufaike na zao hilo la kibiashara.

"Ninaomba kikao hiki kiwe suluhisho la wakulima wa kahawa mnatakiwa kujadili kwa umakini na kutoka na kitu kimoja,ili kujenga ushirika wa haki ambao utamlinda mkulima," alisema Bashe.

Kuhusu ununuzi wa zao hilo, Bashe alisema sekta binafsi inapaswa kununua katika vyama na si kwenda kwa wakulima mmoja mmoja.

### Mbunge aendelea kusota rumande

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MBUNGE wa Kishapu Suleiman Nchambi (CCM), amerudishwa rumande baada ya kesi yake inayomkabili ya tuhuma za uhujumu uchumi kuahirishwa kusikilizwa hadi Mei 25, mwaka huu.

Sababu za kuahirishwa ni Mahakama ya Wilaya ya Shinyanga kutokuwa na uwezo wa kusikiliza kesi za uhujumu uchumi pamoja na utoaji dhamana.

Kesi hiyo ipo chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ushindi Swalo, ambapo kwa mara ya kwanza ilisomwa Mei 8, mwaka huu, na kutajwa kusikilizwa tena jana, na mtuhumiwa kurudishwa rumande.

Mbunge huyo ana shitakiwa kwa makosa 12 ya uhujumu uchumi na kufunguliwa kesi namba 10, 2020, lakini mahakama hiyo haina uwezo wa kusikiliza kesi za uhujumu uchumi wala utoaji wa dhamana.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ofisi za ardhi mikoani ukombozi kwa wengi

**SERIKALI** imetangaza fursa kwa wananchi, baada ya kusema kuwa ofisi za ardhi za mikoa zitaanza rasmi kufanya kazi katika mikoa 26 ya Tanzania Bara mwezi huu.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli kuitaka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuondoa kero na mzigo wa gharama kwa wananchi katika masuala ya ardhi.

Hatua hiyo imeelezwa kuwa ni usogezaji wa huduma za sekta ya ardhi karibu na wananchi sambamba na kuwapunguzia gharama za kufuata huduma hiyo umbali mrefu, ambapo huduma za ardhi awali zilikuwa zikitolewa kwenye ofisi za Ardhi za Kanda na Makao Makuu.

Uamuzi huo ulitangazwa jijini Dodoma juzi na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, na kubainisha kuwa wizara imeanzisha ofisi za ardhi katika kila mkoa ili kutoa huduma zote zilizokuwa zinatolewa kwenye ofisi za kanda au makao makuu.

Alisema, kuanzia sasa wananchi watapata huduma zote katika mikoa yao, na kubainisha kuwa wananchi wa mikoa ya Kigoma na Katavi hawataenda tena Tabora kuchukua hati kama walivyokuwa wakifanya awali huku wale wa Tanga, Manyara na Arusha wakipata huduma katika mikoa yao badala ya kwenda Moshi na wale wa mikoa ya Iringa, Njombe, na Rukwa wakisalia mikoa husika badala ya kwenda Mbeya.

Kwa upande wa wananchi wa mikoa ya Ruvuma na Lindi, hawataenda mkoa wa Mtwara kupata huduma za ardhi na wananchi wa Kagera na Geita nao hawatalazimika kwenda Mwanza, huku wa mikoa ya Mara na Shinyanga wakisalia mikoa yao kupata huduma za ardhi, hivyo hawataenda Simiyu na wale wa Singida na Morogoro wakiepuka kwenda mkoa wa Dodoma kuchukua hati.

Kwa mujibu wa Waziri Lukuvi, nyaraka zote, watumishi pamoja na vitendea kazi tayari vipo mikoani na kubainisha kuwa sasa taasisi kama benki zitaweza kukopesha kwa kasi kwa kuwa dhamana za wakopeshwaji zipo mikoani na masijala za hati zimerudishwa kila mkoa.

Kwa kuzingatia usumbufu ambao wananchi walikuwa wakipata kufuata huduma za masuala ya ardhi nje ya mikoa yao, zikiwamo gharama kubwa, tunaona kuwa hatua hii ya kuwasogezea huduma hizo katika mikoa yao ni ukombozi kwao.

Tunasema hivyo kwa kuwa wananchi wamekuwa wakitumia muda mtefu kusafiri kwenda katika kanda ambako ni mbali, hivyo kutumia gharama za usafiri pamoja na za chakula na malazi, kwa kuwa haiwezekani kwenda siku moja na kurudi.

Kwa hiyo serikali inahitaji pongezi kwa kulitafutia ufumbuzi suala hilo, ambalo limekuwa likiwatesa sana wananchi wengi, ambao uwezo wao kiuchumi ni mdogo.

Kadhalika, hatia hii inathibitisha kuwa serikali inazingatia kuwa masuala ya ardhi zikiwamo changamoto zinawagusa wananchi wengi, hivyo kuona umuhimu wa kuweka mazingira bora ya kutolea huduma husika.


Suala lingine ambalo tunaona kuwa wananchi wamepunguziwa mzigo na usumbufu ni la utoaji wa hati, kutokana na Waziri Lukuvi kusema wasajili wa hati wa mikoa watatoa hati kwa wananchi kupitia ofisi za ardhi za wilaya badala ya wananchi kufuata hati kwenye kanda au mkoani, na kuongeza kuwa, vifaa vya upimaji vimenunuliwa na kusambazwa ofisi hizo za mikoa ili halmashauri za wilaya ziweze kuazima na kupima maeneo yao bila gharama za kuvikodisha.

Tunawapongeza viongozi na watendaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kubadilika na kufanyakazi kwa bidii na ubunifu badala ya mtindo wa zamani wa kufanyakazi kwa mazoea, ambao ulichochea vitendo vya rushwa, ufisadi na kuwakosesha haki wananchi wengi.

Tunaamini kwa kuendeleza utendaji huu, mipango na mingi itatekelezwa, hivyo kuwawezesha Watanzania kunufaika na rasilimali hiyo muhimu kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Chonde chonde likizo hii isiwe chanzo cha mimba

Na Sabato Kasika

**MIMBA** kwa wanafunzi ni tatizo ambalo halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu, kutokana na kuwapo kwa taarifa mbalimbali za kila uchao zinazoonyesha baadhi yao kukatisha masomo kutokana na changamoto hiyo.

Wanafunzi wanaendelea kukumbana na tatizo hilo linalokatisha ndoto zao , huku serikali na wadau wa elimu wakifanya mikakati mbalimbali ya kuwaondoa wasichana kwenye janga hilo.

Lakini imekuwa ikielezwa na wadau wa kutetea haki za watoto na wanawake kuwa mara nyingi mimba hizo hutokea kipindi ambacho wanafunzi wako likizo, hivyo ni wazi kwamba wazazi wanatakiwa kuwa makini.

Imewahi kutokea hata wilayani Liwale mkoani Lindi mwanzoni mwa mwaka huu baada ya wanafunzi kumaliza likizo ya Desemba mwaka jana na kufanyiwa vipimo na kukuta 13 wakiwa na mimba.

Wanafunzi waliopimwa ni kutoka shule 17 za sekondari zilizomo wilayani humo, ambao sasa ni wazi kwamba wamekatisha masomo kutokana na kukutwa na ujauzito.

Kwa hali hiyo, hata wakati huu wa likizo ya corona, wazazi na walezi wa wanafunzi wanatakiwa kuwa makini katika malezi kwa kutowapa uhuru ambao unaweza kusababisha wakajikuta katika mtego wa kupata mimba.

Si kwamba umakini unatakiwa kuwapo kipindi hiki, hapana, bali ni suala la kuzingatiwa wakati wote ili elimu ya makuzi hasa zama hizi ambazo mmomonyoko wa maadili umekuwa mkubwa katika jamii ipewe kipaumbele.

Ni wajibu wa kila mzazi na mlezi kutambua kwamba jukumu la kuelimisha mtoto wake kuhusu madhara ya mimba hizo ili aweze kuziepuka, kuliko kumpa uhuru ambao mwisho wake ni tatizo.

Kila mzazi na mlezi ana wajibu wa kutenga muda kwa ajili ya kutoa elimu ya makuzi kwa watoto wake, akitambua kuwa dunia ya leo imebadilika, hivyo ni muhimu kumsaidia mtoto kwa kila njia ili awe salama.

Hivyo wakati wanafunzi wakiendelea na likizo ya corona ambayo bado haijajulikana itaisha lini, kila mzazi na mlezi atimize wajibu, ili watoto waendelee kuwa salama hadi shule zitakapofunguliwa.

Vinginevyo kama ambavyo inaelezwa na wadau mbalimbali kuwa kuwa likizo nazo zinachangia mimba, basi hata likizo hii ya corona inaweza kusababisha baadhi yao wasirudi shule, kutokana na kupata ujauzito.

Wazazi na walezi wakumbue kuwa zama hizi si za kuona aibu tena, kutokana na ukweli kwamba watoto wa kisasa wanajua mambo mengi mapema, hivyo wakae nao na kuwaambia ukweli kuhusu madhara ya mimba.

Ninatambua kuwa kuna changamoto nyingi zinazochangia mimba za utotoni ukiwamo umaskini, ambao unawafanya watoto washawishiwe kwa kupewa chochote na kujikuta wakishiriki vitendo vya ngono na kupata mimba.

Lakini hali hiyo ya maisha haumzuii mzazi kukaa na mtoto wake na kumwambia kila kitu, kwani hata kama atakuwa mgumu kuelewa, ipo siku atakumbuka kwamba alishaonywa.

Mimba bado ni tatizo kwani katika vyombo vya habari huwa kuna taarifa zinaonyesha wanafunzi wamekatisha masomo kwa sababu ya mimba, hivyo ni kila mzazi na mlezi kutimiza wajibu wake katika malezi.

Elimu ni miongoni mwa haki za msingi za mtoto, hivyo anapokatisha masomo kwa sababu ya mimba anakosa haki hiyo, ndiyo ninasisitiza wazazi na walezi kutenga muda angalau wa nusu saa mara moja kwa siku kwa kukaa na watoto.

Si kukaa tu bali kukaa nao kitako na kuwapa elimu kuhusu madhara ya mimba hizo za utotoni na bahati nzuri watoto wao wapo likizo, kwa hiyo hata wale wanaosoma shule za bweni wapo nyumbani.

> **Hivyo wakati wanafunzi wakiendelea na likizo ya corona ambayo bado haijajulikana itaisha lini, kila mzazi na mlezi atimize wajibu, ili watoto waendelee kuwa salama hadi shule zitakapofunguliwa.**

Walimu wamekuwa wakijitahidi kuelimisha wanafunzi kwa undani kuhusu mimba kwenye masomo ya bailojia ni vyema wazingatie ili iwasaidie kutambua madhara ya kiafya yanayotokana na mimba za utotoni.

Lakini utoaji wa elimu ya afya ya uzazi na makuzi ni ya muhimu kuanzia nyumbani na hata kwenye jamii nzima ili likizo hiyo iwaepushe wanafunzi na tatizo la corona na mimba za utotoni.

# Wawili wakabiliwa kesi uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

WATU wawili akiwamo Mwandishi wa Habari wa gazeti la Jamhuri, Angellah Kiwia(41) na dereva Mohamed Rushaka (36), wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo mashitaka manne ya kuongoza genge la uhalifu, kuteka nyara na kutakatisha Sh.milioni 30.

Washitakiwa hao walisomewa mashitaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali, Esther Martin, alidai washitakiwa hao wanakabiliwa na mashitaka manne.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa katika shitaka la kwanza, washitakiwa wanadaiwa kati ya Machi Mosi na Machi 31, mwaka huu, katika mahali tofauti jijini Dar es Salaam, kwa makusudi waliongoza genge la uhalifu kwa lengo la kujipatia faida.

Katika shitaka la pili, siku ya tukio la kwanza washitakiwa walimteka Seleman Mohamed, wakiwa na lengo kumpeleka katika eneo la hatari ya kumuumiza.

Martin alidai kuwa washitakiwa hao wakiwa na lengo la kulipwa isivyo halali walidai Sh. milioni 30 kutoka kwa Mohamed, baada ya kumtishia kumuua.

Katika shitaka la nne, siku na eneo la tukio walijipatia Sh. milioni 30 kutoka kwa Mohamed, huku wakijua kuwa fedha hizo ni zao la makosa tangulizi la kuratibu genge la uhalifu na kutekwa nyara.

Washitakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi bado haujakamilika na kuomba mahakama kupanga tarehe ya kutajwa.

Hakimu Chaungu alisema kesi hiyo itatajwa Mei 25, mwaka huu na washitakiwa wapelekwe mahabusu.



Mchuuzi wa mananasi na maboga akiwa ameisheheni baiskeli yake wakati akitafuta wateja katika eneo la Buguruni, Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam jana. Maboga hutumika sana katika maandalizi ya futari hasa katika kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Polisi yaua majambazi wanne

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

JESHI la Polisi limewaua majambazi wanne baada ya kurushiana risasi eneo la Maragarasi, Kijiji cha Mvugwe, kitongoji cha Kanpe, Wilaya ya Kasulu, mkoani Kigoma.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Martini Otieno, alisema tukio hilo limetokea jana saa 12 alfajiri, baada ya kupata taarifa majambazi wanane wamejipanga kufanya utekaji katika eneo la Maragarasi upande wa Kasulu katika barabara ya Kasulu-Kibondo.

Otieno alisema kwa bahati nzuri askari walikuwa wamejipanga na walipofika katika hilo eneo, majambazi hao waligundua kwamba askari wameingia katika eneo hilo na kuanza kurusha risasi.

Alisema katika tukio hilo majambazi wanne waliuawa palepale na wengine wanne walikimbilia porini na kutokomea.

Kadhalika alisema katika tukio hilo walifanikiwa kupata bunduki moja ya kivita aina ya AK 47 ikiwa na risasi 13 ndani ya magazine, pia kulikuwa na risasi zingine 40 zimewekwa kwenye mfuko na mapanga mawili na mkuki mmoja.

Kwa mujibu wa Kamanda Otieno, kuna tukio jingine ambalo lilitokea Mei 8, mwaka huu, raia wanne waliwakamata maeneo ya Wilaya ya Kasulu maeneo ya Kwa Shayo, wakiwa wanamiliki kinyume cha utaratibu bunduki aina AK 47 yenye namba TX87101996 na watuhumiwa hao ni Yolamu Hamisi, Aberi Ngoma, Alesi Yolamu (63) na mwanamke Asha Hamisi.

Alisema watuhumiwa hao walipatikana na silaha AK 47 pamoja na risasi 49 na magazine mbili na moja ilikuwa na risasi 30 na magazine nyingine ikiwa na risasi 19.

Alisema mtuhumiwa Ally Hamisi ambaye ni mtoto wa mwanamke huyo anatafutwa na polisi kwa madai ni jambazi sugu. "Tulikuwa tukimtafuta kwa muda mrefu na ndiye alikuwa ameleta hiyo silaha na kuificha kwenye nyumba yao na mama yake alifahamu hilo tukio, lakini hakuchukua tahadhari wala kutoa taarifa katika vyombo vya ulinzi na usalama."

Kamanda Otieno aliwataka wananchi wakimuoa jambazi huyo maarufu kwa jina la Pima ajisalimishe kituo chochote cha polisi.

# Vodacom yaridhishwa ongezeko umiliki soko

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Vodacom, imetoa matokeo ya awali ya kifedha kwa mwaka, unaoishia Machi 31, mwaka huu, ikionyesha ukuaji wa kibiashara unaodhihirishwa na ongezeko la umiliki wake wa soko kufikia asilimia 32.8.

Mafanikio hayo yametokana na kuongeza idadi ya wateja wake wapya milioni 1.4 na kufikisha jumla ya wateja milioni 15.5.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom, Hisham Hendi, wakati akizungumzia matokeo ya jumla ambayo yamehusisha ukuaji wa mapato wa asilimia 0.9 kutokana na utekelezaji thabiti wa mikakati ya kibiashara unaowezeshwa na ukuaji wa idadi ya wateja.

Alisema ukuaji mdogo katika nusu ya pili ya mwaka kwa sehemu kubwa ulitokana na matokeo ya kufungia wateja milioni 2.9 ambao hawajasajiliwa kwa kutumia alama za vidole na gharama zinazohusiana na kukidhi miongozo ya mamlaka pamoja na ushindani mkubwa wa bei.

"Wateja wetu wanaendelea kunufaika na mtandao bora wa kiwango cha juu wa Vodacom kutokana na uwekezaji mkubwa wa Sh. bilioni 154.6 katika kuongeza upatikanaji wa mtandao wa 4G na kuboresha ubora wa mtandao na huduma zetu," alisema Hendi.


Alisema, kufuatia kuboreshwa kwa huduma za malipo ya kidijitali; Mapato ya M-Pesa yameripotiwa kuongezeka kwa asilimia 7.4 ambayo imechangia asilimia 35.0 katika mapato ya huduma kufikia 2.2pp inayotokana na kuongezeka kwa idadi ya miamala kwa kila mteja.

"Huduma yetu ya M-Pesa imeendelea kutimiza ahadi yake ya kuleta ushirikishwaji wa kifedha nchini, kuwawezesha wateja kufanya miamala kwa urahisi na kuchangia katika kukua kwa uchumi. Kwa sasa tuna wateja milioni 10.1 wanaotumia huduma hii ya M-Pesa ambao wamefanya miamala bilioni 1.4 yenye thamani ya Sh. trilioni 58.1 katika mfumo wa huduma za kifedha kupitia simu za mkononi kwa mwaka," alisema Hendi.

Alifafanua kuwa, Vodacom itaendelea kupanua mfumo wa M-Pesa kwa kutoa huduma zaidi ili kukidhi mahitaji ya sasa ya wateja kwa kadri yanavyoendelea kubadilika.

Alisema kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19 ambao unaathiri mataifa na wananchi duniani kote, kipaumbele cha Vodacom ni katika afya na usalama wa wafanyakazi wao wakati wakitoa huduma na msaada kwa wateja wao pamoja na kusaidia serikali pale inapowezekana, kwa ajili ya kukabiliana na hali ya ugonjwa huo.

BURIANI



# Mbuyu wa uandishi, Fili Karashani, umeanguka

**Na Kajubi Mukajanga**

SAA 6.21 mchana wa Jumapili, Mei 10, 2020 nilizungumza na Kagina Karashani kuhusu maendeleo ya matibabu ya baba yake, Fili, na mipango ya kumtembelea hospitali katika mazingira ya homa kali ya mapafu (Covid-19) yaliyofanya uongozi wa Hospitali ya Muhimbili (MNH) kuamua awe anaonwa na mtu mmoja tu kwa siku!

Alikuwa amelazwa Muhimbili kwa matatizo ya moyo ambayo yamekuwa yakimsumbua kwa muda wa miaka kadhaa.

Saa sita baadaye, saa 12.23, nikapokea simu ya Kagina: "Habari ni mbaya. Mzee amefariki."

Nilimfahamu Fili Karugahale Karashani kama rafiki mcheshi, rafiki wa kifamilia, mtu wa masihara ambaye katika nyakati za furaha alinihakikishia kuwa ataandika wasifu wangu pindi nitakapofariki. Nilikuwa nikimjibu kuwa mimi ndiye nitakayeandika wa kwake. Na sasa nauandika.

Nilimfahamu pia kama mwanataaluma mahiri wa uandishi wa habari, na mkufunzi bora. Kabla sijawa Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), tulizunguka nchi nzima kufundisha maadili ya uandishi, stadi za uongozi katika klabu za waandishi, mbinu za uandishi wa uchunguzi, uandishi wa habari za uchaguzi na uandishi wa makala.

Machi 30, 2012, Fili, kama anavyojulikana kwa wengi, alikuwa mtu wa kwanza kutunukiwa Tuzo ya Maisha ya Mafanikio katika Tasnia ya Habari (Lifetime Achievement in Journalism Award) ambayo alikabidhiwa na Rais mstaafu Jakaya Kikwete katika Ukumbi wa Diamond Jubilee. Tuzo hizo huandaliwa na MCT na washirika wake, na hutolewa katika kilele cha Tuzo za Umahiri katika Uandishi wa Habari nchini, EJAT.

Alikuwa mmoja wa wanahabari Watanzania ambao usingeweza kuongelea uandishi wa habari uliotukuka bila kuwataja. Nguli huyu alikuwa katika taaluma hii kwa miongo mitano kama ripota, mwandishi wa makala, mhariri, mkufunzi, mtafiti na mtaalamu mshauri wa masuala ya habari hapa nchi na ughaibuni. Kwa maneno yake mwenyewe, alijinasibu: "I am a child of the Media" (Mimi ni mtoto wa Tasnia ya Habari).

Fili alianza maisha ya kazi kama msaidizi wa duka la vitabu mjini Dodoma mnamo mwaka wa 1960, ambapo alijenga tabia ya kujisomea, na baadaye, kuandika. Akahudhuria warsha ya uandishi wa habari huko Kiomboi, mkoani Singida, iliyoandaliwa na Christian African Writing Centre iliyokuwa na makao makuu Kitwe, Zambia, na kumaliza akiwa mwanafunzi bora darasani. Ushindi huo ulimwezesha kupata udhamini wa kusomea Cheti cha Uandishi huko Kitwe, akiwa mmoja wa vijana 30 waliokusanywa kutoka kusini, mashariki na magharibi mwa Afrika. Baada ya kupata cheti chake akaajiriwa kama ripota katika magazeti ya Target na Lengo, ambayo yalikuwa ndiyo kwanza yameanzishwa kwa ushirikiano kati ya mabaraza ya Kikristo ya Kenya na Tanzania.

Miaka miwili baadaye mwajiri wake akampeleka kusomea Diploma ya Uandishi iliyoandaliwa na taasisi ya kimataifa ya wahariri, International Press Institute. Kwa mara nyingine, Fili akawa wa kwanza katika darasa la wanafunzi 30 toka kusini na mashariki mwa Afrika. Wakati wa sherehe za mahafali, Mhariri wa Taifa Leo, linalochapishwa na Nation Media Group (NMG) ya Kenya akamfuata na kumweleza kuwa angependa kumpa kazi. Fili akakubali. Hiyo ilikuwa mwaka 1964. Miezi mitatu tu baadaye, wahariri wa Daily Nation, gazeti jingine la NMG, "wakamwiba" toka gazeti lao dada. Akaingia chumba cha habari cha gazeti lao la Kiingereza akiwa Mtanzania pekee.

Tangu hapo, Fili hakuwahi kutazama nyuma.

Kwa Fili, ukweli na usahihi (truth and accuracy) ndiyo msingi wa uandishi wa habari. Mhariri wake wa habari pale Daily Nation, Mike Chester, alikuwa kati ya watu waliosaidia kumfinyanga Fili kuwa gwiji wa taaluma hiyo. Chester hakuwa na masihara kazini, na kwake, stori ilikuwa haijakamilika bila kujibu maswali "kwa nini" na "kwa jinsi gani".

Kati ya kazi alizofanya wakati huo ni pamoja na kuripoti machafuko ya kijamii, ukame na njaa huko Wajir, mpakani mwa Kenya na Somalia. Baadhi ya stori alizoandika zilimuudhi aliyekuwa Waziri wa Kilimo wa Kenya wakati huo, Jeremiah Nyagah. Lakini ukweli na usahihi ukamwokoa, hakufanywa chochote.

Aliandika pia matatizo ya wananchi huko Baringo, jimboni kwa Daniel Arap Moi, wakati huo akiwa Makamu wa Rais na Waziri wa Mambo ya Ndani. Mzee Moi hakupendezwa sana na stori za Fili, na akaagiza aletwe kwake. Alipofika, akamtazama Fili kwa mshangao toka chini hadi juu na kumaka, "Oh, huyu ndiye Karachani - nilidhani ni Mhindi! Kwenda!"

Awali, lengo lilikuwa kumsweka korokoroni. Ukweli na usahihi vikamwokoa.

Tom Mboya alipouawa, Fili ndiye aliyeliandikia Daily Nation mkasa huo.

Mwaka 1967 akahamishiwa Dar es Salaam kwa mwaka mmoja na kuendelea kupeleka Nairobi stori kemkem. Asilimia kubwa ya stori za Tanzania zilizochapishwa ukurasa wa mbele wa Daily Nation wakati huo ziliandikwa na Fili.

Aliporudi Nairobi, Fili alikwea vidato toka ripota hadi mwandishi mkuu wa habari za Bunge, akawa pia mwanasafu, na baadaye Mhariri-usu/Msanifu Habari (Sub-editor). Alikuwa pia akiandika safu kuhusu masuala ya Tanzania katika gazeti hilo lililoongoza kwa mauzo Afrika Mashariki.

Baadaye akaacha kazi na kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar e Salaam na kupata shahada yake ya kwanza mwaka 1978, kisha shahada ya uzamili toka Chuo Kikuu cha Queens, Canada, mwaka 1981.

Baada ya chuo kikuu Fili akajiunga na gazeti la Daily News kabla ya kuwa mkufunzi katika Chuo cha Uandishi wa Habari Tanzania, TSJ. Akiwa mkufunzi, akawa pia akiandikia majarida na taasisi za nje zikiwamo jarida maarufu la Africa Now na shirika la Inter Press News Agency (IPS). Kwa bahati mbaya, jambo hili lilitafsiriwa na wakubwa wake kuwa ni "kufanya kazi mbili", japo kwake yeye aliona ni njia ya kuwaonyesha wanafunzi kwa vitendo jinsi uandishi bora ulivyo. Alipoona anasakamwa sana, akaacha kazi na mara moja IPS wakamchukua na kumpa kazi Roma, Italia, na baadaye wakampeleka Harare, Zimbabwe, kama Mkuu wa Kituo (Bureau Chief).

Aliporudi Tanzania 1989 akawa Mhariri mwanzilishi wa Business Times, akiwa na kina Rashid Mbuguni, Narendra Joshi, Ali Chimbyangu na Richard Nyaulawa.

Mwaka 1991 Fili Karashani aliajiriwa kama Mhariri wa Southern Africa Economist jijini Harare, kabla ya kurudi Dar es Salaam na kuwa Mhariri mwanzilishi wa The Guardian na baadaye Sunday Observer.

Mnamo 2004 hadi 2005 alikuwa The Citizen kama Mhariri wa Mafunzo.

Katika miaka ya mwisho ya maisha yake, Fili Karashani, ambaye waandishi wengi wamepitia mikononi mwake akiwa mhariri na mwalimu, aliendelea kutoa mafunzo ya uandishi, hususan uandishi wa habari za uchunguzi, makala, na maadili. Alitoa pia huduma kama mtaalamu mshauri wa masuala ya habari, huku akichangia katika majarida ya kitaaluma yakiwamo Scribes la MCT na The Global Journalist la Shule Kuu ya Uandishi wa Habari ya Chuo Kikuu cha Missouri, Marekani.

Vitabu alivyoandika au kushiriki kuandika ni pamoja na: To Write or Not to Write - Ethical Concerns in Journalism; Poverty Reporting - A Manual for Tanzanian Journalists; Media Ethics: Duties and Responsibilities; Feature Writing Manual na Investigative Journalism Practice in Tanzania.

Fili Karashani alipata kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wanahabari wa Kenya (Kenya Union of Journalists) na katika miaka yake ya mwisho alikuwa mwenyekiti wa Kituo cha Habari, Tanzania Press Centre kabla ya kupatwa na matatizo ya kiafya.

Fili Karashani alizaliwa Agosti 23, 1938 mjini Dodoma. Baba yake alikuwa Yakobo Kagina, mchungaji wa kanisa la Anglikana, na mama yake aliitwa Blandina.

Fili na mkewe, Geraldina, walijaaliwa watoto watano: Magezi, Baraka, Kagina, Koku na Bahati. Baraka, aliyechukua kazi ya baba yake ya uanahabari, alishatangulia mbele ya haki. Fili pia ameacha wajukuu wanane.

**HABARI KITAIFA**

# Uvaaji wa barakoa bado tatizo Mafia

**Na Yasmine Protace, KIBITI**

IMEELEZWA kuwa baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Kibiti mkoani Pwani, hawana uelewa wa uvaaji halisi wa barakoa.

Mbali ya kutokuwa na uelewa wa uvaaji wa barakoa, pia kuna baadhi ya watu ambao wanaendelea kukaa katika mikusanyiko ambayo serikali imeizuia kutokana na kuwapo kwa maambukizo ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19.

Hayo yalisemwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Kibiti katika kikao cha Baraza la Madiwani.

Alisema pamoja na wilaya kutoa elimu ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona, lakini kuna baadhi ya watu elimu hiyo hawaitilii maanani.

"Tunawapatia elimu jinsi ya kujikinga na maambukizo ya corona, tunawaambia uvaaji wa barakoa, kunawa mikono, kutumia vitakasa mkono, lakini baadhi ya watu unawaona kabisa hawatilii maanani uvaaji wa barakoa," alisema.

Aliongeza kuwa wataendelea kutoa elimu ambayo itawasaidia jinsi ya kupambana na maambukizo ya corona.

Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Gulam Mukusini Faki, alisema kuwa elimu iendelee kutolewa na wanaotoa elimu wawe wanavaa barakoa.

Alisema wale ambao wataendelea kukaa vijiweni, watakamatwa na kufikishwa katika ofisi za halmashauri, hospitali, polisi na sokoni kwa ajili ya kufanya usafi na jioni wataruhusiwa kwenda makwao.

"Kwa kufanya hivyo, kunaweza kupunguza idadi ya watu wanaopenda kukaa vijiweni," alisema.

**"Tunawapatia elimu jinsi ya kujikinga na maambukizo ya corona, tunawaambia uvaaji wa barakoa, kunawa mikono, kutumia vitakasa mkono, lakini baadhi ya watu unawaona kabisa hawatilii maanani uvaaji wa barakoa," alisema.**

# Diwani mbaroni tuhuma kumfanyia vurugu DC

**Na Neema Hussein, KATAVI**

JESHI la Polisi mkoani Katavi linamshikilia Diwani wa Kata ya Ikuba, Emmanuel Washeri (43), kwa tuhuma za kuhamasisha kundi la vijana kumfanyia fujo Mkuu wa Wilaya ya Mlele, Rachel Kasanda, baada ya kukamata gari aina ya Fuso likipakia magunia ya ufuta nyumbani.

Diwani huyo anadaiwa kufanya hivyo kinyume cha taratibu zilizowekwa na uongozi wa wilaya hiyo.

Tukio hilo lilitokea katika Kijiji cha Kashishi Wilaya ya Mlele mkoani humo, ambapo askari polisi wakiwa na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo wakifuatilia taratibu mpya zilizowekwa na kila wilaya kuhusiana na mazao kuuzwa kwenye vituo maalumu, hivyo walifanikiwa kukamata gari hilo namba T.924 DNE likiwa na magunia 83 ya zao la ufuta.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Benjamin Kuzaga, alisema gari hilo lilikuwa likiendeshwa na Yusuph Zephania, mkazi wa Sumbawanga mkoani Rukwa.

Kuzaga alisema wakiwa nyumbani kwa diwani huyo, lilitokea kundi la vijana likiongozwa na watu wawili ambao ni Mwandu Ngaliga (25) na Bida Charles (28), ambalo lilihamasishwa na diwani na kuanza kufanya fujo kwa kuwarushia mawe viongozi hao na askari.

Kamanda huyo alisema vurugu hizo zilisababisha askari kuwatawanya kwa kufyatua risasi nne za moto hewani na mabomu matatu ya kishindo ili kumwokoa mkuu wa wilaya na viongozi wengine.

Kwa mujibu wa Kamanda Kuzaga, gari la DC liliharibiwa baadhi ya vifaa na kwamba thamani ya uharibifu huo haijafahamika.

Alisema mbali na diwani huyo, pia wanawashikilia watu walioongoza vurugu hizo pamoja na gari hilo likiwa na magunia ya ufuta na kwamba upelelezi ukikamilika watafikishwa mahakamani.

Hivi karibuni Mkoa wa Katavi ulitangaza vituo maalumu kwenye kila wilaya vya kuuzia mazao pamoja na mazao yanayotakiwa kuuzwa kwenye vituo hivyo. Mazao hayo yanayotakiwa kuuzwa kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani ni ufuta na alizeti.



Mwenyekiti wa Masjid Al-waahabu ya mjini Kahama, Ahmed Haroun Alnoobiy, akikabidhi mfuko wa sukari wa kilo 25 kwa Mkuu wa Gereza la Kahama, Misana Shigumha, uliotolewa na Jumuiya ya International Istiqaama Muslimu Community ya Oman, kwa ajili ya wafungwa na mahabusi Waislamu, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# DED ataka watumishi kuvaa barakoa

**Na Hamisi Nasiri, MASASI**

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Masasi, mkoani Mtwara, Changwa Mkwazu, amewataka watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, kuvaa barakoa kila wanapowahudumia wananchi katika kujikinga na corona.

Akizungumza na wajumbe wa kamati ya lishe ya halmashauri hiyo katika kikao cha lishe, alisema watumishi wote wanapaswa kufuata maelekezo ya watumishi wa afya.

Alisema katika mapambano ya kujikinga na maambukizo ya corona kila mtumishi wa halmashauri hiyo lazima ahakikishe anavaa barakoa anapokuwa ofisini kwa ajili ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huo.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Afya imekuwa ikisisitiza kila siku jamii kuchukua hatua za kujikinga na virusi vya corona, na kwamba kuna kila sababu kwa watumishi kuonyesha mfano kwa kuwa mstari wa mbele kuzingatia maelekezo hayo yanayotolewa na serikali.

Mkwazu alisema kuanzia sasa anaagiza kila mtumishi wa halmashauri hiyo kuvaa barakoa anapokuwa kazini na pia kufuata maelekezo yote ikiwamo kujitakasa mikono.

Alisema watumishi hao wamekuwa wakikutana na watu mbalimbali wanaokuja kwenye ofisini zao kufuata huduma mbalimbali na kwamba, iwapo hawatozingatia kanuni za kujikinga na corona basi wanajiweka katika hatari ya kuambikizwa corona.

"Nataka nione kila mtumishi hapa ndani anavaa barakoa anapofika hapa kazini na awe amevaa muda wote anapokuwa anahudumia wananchi, sisi watumishi ndio tunakiwa kuwa mstari wa mbele kuchukua hatua zote za kujikinga na corona," alisema Mkwazu.

Aidha, mkurugenzi huyo aliwataka watumishi hao na jamii kwa ujumla kujenga utamaduni wa kupenda kula matunda na vyakula vyenye lishe bora kwa afya ya mwili hasa katika kipindi hiki cha uwapo wa ugonjwa wa corona.

Alisema uwapo wa kinga thabiti ya mwili kunasaidia kuwaepusha kupata baadhi ya magonjwa, na kwamba magonjwa hayo yanashindwa kupata nafasi ndani ya mwili kwa sababu kinga ya mwili inakuwa ipo thabiti.

Mkwazu alisema kinga thabiti inatokana na ulaji wa vyakula bora vyenye kuzingatia lishe bora kama mboga za majani pamoja na ulaji wa matunda kwa wingi kama ndizi, machungwa na mapapai ni muhimu kwa afya ya binadamu.

Ofisa Habari wa Hamashauri hiyo, Joina Nzari, alisema utekelezaji wa agizo hilo umeshaanza kwa kuwa baadhi ya watumishi wameanza kuvaa.

HABARI BUNGENI

# Njia ya Mlima Kilimanjaro kuongeza mapato ya utalii

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WIZARA ya Maliasili na Utalii imesema kufungua njia ya Kidia itakayotumika kwa wageni maarufu (VIP) watakaokuwa wanapanda Mlima Kilimanjaro itaongeza mapato ya serikali kupitia utalii.

Hayo yalibainishwa jana bungeni na wizara hiyo ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Esther Mmasi (pichani).



Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji uzinduzi wa VIP kwa wageni wanaopanda mlima huo na kudai kuwa wananchi wa Kata ya Old Moshi Mashariki kwa muda mrefu sasa wamekuwa wakisubiri uzinduzi wa njia hiyo.

"Je, kwa nini serikali isione umuhimu wa kutekeleza azma hiyo iliyodumu kwa muda mrefu sasa?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, Sh. milioni 200 zimetengwa kwa mwaka 2019/2020, kwa ajili ya kufungua njia hiyo yenye urefu wa kilometa 25 ambapo kwa sasa kazi inaendelea.

Aidha, ilisema kiasi cha shilingi milioni 230 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya kupokea na kuhudumia wageni, lango pamoja na kutengeneza njia (trail) ya kupandia mlima kuanzia Kidia.

Wizara hiyo ilisema kuwa kuzinduliwa kwa njia hiyo, kutaongeza mapato ya serikali kupitia utalii, lakini kutaongeza fursa kwa wananchi wa Kata ya Old Moshi Mashariki kufanya biashara kwa watalii, mawakala wa utalii na watoa huduma ya utalii watakaokuwa wanatumia njia hiyo.

"Wizara kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) ilishaona umuhimu wa kufungua njia ya Kidia itakayotumika kwa wageni maarufu (VIP) watakaokuwa wanapanda Mlima Kilimanjaro," ilisema.

Ilibainisha kuwa kutokana na umuhimu wa njia hiyo, shirika limeiweka kwenye Mpango wa Jumla wa Usimamizi wa Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro (General Management Plan - GMP) wa mwaka 2016 - 2026.

# Watoa huduma afya wahimizwa mwongozo

SERIKALI imewataka watoa huduma wote wa afya nchini kutumia mwongozo wa matumizi ya dawa aina ya 'Misoprostol' ili kuboresha huduma za afya ya uzazi na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Maelekezo hayo yalitolewa jana bungeni na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Hawa Mwaifunga (pichani).

Katika swali lake, mbunge huyo alisema dawa hizo hutumika kwa ajili ya matatizo ya kinamama na kuhoji, serikali ina mpango gani wa kurasimisha matumizi ya dawa hiyo.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema inaendelea kusimamia utekelezaji wa juhudi mbalimbali za kuboresha huduma za afya ya uzazi na mtoto ikiwamo upatikanaji wa dawa muhimu ikiwa na lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga nchini.

Hata hivyo, ilisema serikali imesharasimisha matumizi sahihi ya dawa hizo kwa kuandaa mwongozo ambao umeanza kutumika nchini Julai mwaka jana.

Ilibainisha kuwa mwongozo huo ni juu ya matumizi bora ya dawa muhimu kwa wajawazito wakati na baada ya kujifungua ili kuendana na lengo hilo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga nchini.

"Katika mwongozo huu, mojawapo ya dawa iliyoainishwa ni matumizi ya Misoprostol ambapo dawa hii ni ya mstari wa tatu (third line), dawa aina ya Oxytocin ikianza, ikifuatiwa na dawa aina ya Ergometrine halafu ndio dawa ya Misoprostol," Wizara hiyo ilifafanua katika majibu yake kwa mbunge huyo.

Aidha, ilisema matumizi ya dawa hiyo ni kwa ajili ya kutoa huduma muhimu baada ya mimba kuharibika, kuanzisha uchungu kwa wajawazito ambao wamepitiliza muda wao wa kujifungua na kukinga na kutibu utokaji wa damu nyingi baada ya kujifungua.

"Nachukua fursa hii kuwataka watoa huduma wote wa afya nchini kutumia mwongozo huu ili kuwezesha kuboresha huduma za afya ya uzazi, kwa pamoja tunaweza kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.



# Utaratibu ujenzi ukuta wa bahari Mtwara waelezwa

BUNGE limeelezwa kuwa ukuta wa bahari eneo la Ruvula Mtwara unapaswa kujengwa kwa mawe ili kukinga mawimbi yasielekee upande wa bomba na mtambo wa kuchakata gesi asilia ya Mnazi Bay.

Wizara ya Nishati ilitoa ufafanuzi kuhusiana na utaratibu huo wa ujenzi bungeni jana katika swali la Mbunge wa Mtwara Vijijini (CCM), Hawa Ghasia (pichani), ambaye alihoji ni lini serikali itaanza kujenga ukuta huo ili kuvilinda visima vya gesi vya Mnazi Bay.

Katika majibu yake, wizara hiyo ilisema mwaka 2017 serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa kushirikiana na Kampuni ya Maurel & Prom (M&P), ilifanya utafiti wa kina katika eneo hilo.

"Lengo ni serikali kupata mapendekezo na ushauri wa kitaalamu kuhusu namna bora ya kuimarisha ufukwe huo, ambapo taarifa za awali za utafiti zinapendekeza kujengwa kwa ukuta wa mawe," ilisema.

Ilisema serikali inakamilisha uchambuzi wa taarifa ya utafiti huo na kazi za kudhibiti mmomonyoko huo zinategemea kuanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/21.

Awali, ilifafanua kuwa tatizo la mmomonyoko wa ardhi katika ufukwe wa Mnazi Bay lilitokea kwa mara ya kwanza Januari, 2015 baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha mawimbi makali ya bahari, ambayo yalisomba kipande cha ufukwe chenye upana wa takribani mita mia moja.

Ilieleza kuwa katika hatua za muda mfupi za kutatua tatizo hilo, serikali kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mtwara ilijaza mawe katika eneo hilo kwa lengo la kudhibiti mmomonyoko huo.



Nipashe
# TESA
Jumanne Mei 12, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Mapinduzi elimu yanautegemea mkopo huu wa Benki ya Dunia**



Ukurasa 13

Janga la corona na tafakuri ya uwezo, ukuu wa Mungu



Ukurasa 12

**Baada ya corona kutishia kambi za taaluma mkoa waibuka kivingine**

SAYANSI

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Simu za mikononi kitisho kingine uhai, mazingira

MIAKA 47 iliyopita simu ya mkononi iligunduliwa . Ni kazi iliyofanyika mwaka 1973 na timu ya wataalam wafanyakazi wa kampuni ya Motorola wakiongozwa na mtafiti na mgunduzi Dk. Martin Cooper.

Mbobezi huyu aliitumia simu ya mkononi kwa mara ya kwanza Aprili 1973 na kuandika historia mpya duniani.

Aidha, matumizi ya simu hiyo yalifungua mlango na soko la bidhaa hizo sehemu mbalimbali duniani na hata leo ni sawa na kusema ina umuhimu wa kipekee si kwa watu binafsi bali kwa taasisi zote duniani zikiwamo serikali.

Leo matumizi ya simu hizo yamekuwa makubwa hasa kwa mataifa yanayoendelea pamoja na Tanzania. Ongezeko la simu linamaanisha ukubwa wa ongezeko la uchafu utokanao na simu pale matumizi yanapomalizika na hivyo kuchangia katika uchafuzi hatari na mkubwa wa mazingira duniani hasa nchi masikini.



Simu na vifaa au viambato vyake, kutupwa kiholela bila kufanyiwa urejelezaji ni kitisho kwa binadamu na mazingira. **PICHA: MTANDAO**

Ni kutokana na kuleta tatizo la namna ya kutupa mabaki ya simu kuanzia betri, vioo, madini na viambato vyote muda unapomalizika.

Kwa kuangalia ukubwa wa tatizo hili na athari za haraka zinazotishia bayoanwai, Nipashe imefanya uchambuzi wa madhara ya simu na viambata vyake na mbinu za kutumia ili kuepusha kitisho kikubwa kinachokuja.

Ni wazi kuwa betri za simu za mikononi zinazotupwa kila mahali bila kujua kuwa ni suala lenye athari kwa Watanzania na mazingira. Wengi watakubaliana nasi kuwa simu hizi na viambato vyake hutupwa ovyo pasipo na utaratibu maalum. Ukiacha matatizo ya kimazingira yanatokanyo na simu yenyewe, pia betri zake zinatupwa bila mpangilio.

Aidha, simu ya mkononi inaonyesha kuwa kwa wastani asilimia 45 imeundwa kwa plastiki.

Pia kwa asilimia 40 ni nyaya, asilimia nne ni ute mkavu na zilizobakia 11 ni madini ya metali mbalimbali.

Madini mengi katika simu hizi kwa mujibu wa taaarifa za mtandao yana sumu kali mfano madini ya risasi na mengine yasiyo na majina ya Kiswahili mfano brominated flame -retardants, beryllium, chromium arsenic, antimony na cadmium. Ni hatari sana mtandao unaonya.

Kwa mujibu wa mitandao ya taarifa za kuunda simu na teknolojia ya mawasiliano ya kielektroniki, betri ya simu imeundwa mahususi kubadilisha nguvu ya kikemikali iliyomo ndani yake na kuifanya iwe nguvu ya umeme.

Kwa hiyo nguvu yake hutegemea kemikali iliyomo ndani yake ambayo ikiwa hasi ndipo betri inaweza kufua umeme na pale inapofikia sifuri haina uwezo wa kufua umeme, ndipo wazo la kuichaji linapoanza.

Katika hali hii kinachotumiwa ni nguvu ya nje ya betri kuirudishia uwezo wa kufua umeme kwa hiyo betri huchajiwa ili kuipa tena nguvu ya kuzalisha umeme huo, ndiyo maana zinachajiwa kila nguvu zinapoisha.

Ni wazi kuwa namna ya kutupa betri ya simu ni changamoto kubwa kwa kila sehemu nchini licha ya kwamba zina metali nzito kama mercury, lead, cadmium na nickel na kwa hiyo utupaji holela unaharibu mazingira na kutishia usalama wa bayoanuia.

Mathalani, kama kawaida betri hizi hutupwa jalalani na watoto huzichezea, zikichomwa baadhi ya metali zinaiweza kuingia kwenye hewa, nyingine zilizoko kwenye majivu huingia ardhini na kwenye mazingira na maji pia. Mitandao inaeleza kuwa uharibifu huu wa mazingira unaweza kusababisha magonjwa mbalimbali yatokanayo na athari za metali hizi zinazokwenda moja kwa moja kwenye mimea wanyama na viumbe wengine.

Utupaji betri unatakiwa kutazamwa kwa upana na kwa makini ikiwezekana Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi Mazingira (NEMC), Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) na wadau wengine waweke utaratibu wa kudhibiti utupaji wa betri na simu zilizoisha muda wake.

Kadhalika kuna haja ya kutumia sheria za kimataifa kama vile The Basel Convention, ambayo Tanzania imeridhia katika kudhibiti utupaji wa simu na viambata vyake.

### CHANZO CHA MARADHI

Mitandao inaeleza kuwa risasi au 'lead' ipo katika kundi hatarishi la kemikali zinazojikusanya kwenye seli za viumbe kidogo kidogo na kuleta madhara makubwa kwani risasi ipo kwenye orodha ya PBTs na inajulikana kuwa ni sumu mbaya sana kwa wanadamu, viumbe wengine na mazingira kwa ujumla.

Inakuwa na athari kubwa kwani inaweza kuharibu mfumo mzima wa kiikolojia na kwa binadamu, baadhi ya athari zake ni kwenye mfumo wa mishipa ya fahamu ambapo inaharibu mishipa mkuu ya neva, inaharibu kinga ya mwili, figo, inadumuza ukuaji wa ubongo kwa watoto na hivyo kupunguza uwezo wao wa kuelewa na akili kufanyakazi ipasavyo inaweza kusababisha saratani na madhara mengine mengi .

### SUMU KUJIKUSANYA MWILINI

Katika simu ya mkononi vizuio vya moto 'brominated flame retardants (BFRs)' hupatikana katika plastiki la jumba la simu ambalo wengi huliita 'hauzing' ili kuzuia kuungua simu endapo itashika moto. Aina mbalimbali ya BFRs zinazotumika ni malighafi za 'polymeric' zenye madhara makubwa ya kiafya kwa binadamu na mazingira.

Utafiti unaonyesha kuwa BFRs, polymeric ni sumu zinazojikusanya kwenye mfumo wa viumbe hai na kukaa muda mrefu hivyo simu za mikononi kutupwa kwenye madampo kusogeza hatari hiyo kwa viumbe hai wanaoishi karibu .

Baadhi ya hizi kemikali kama vile Polybrominated diphenyl zinahusishwa na uwezekano wa kusabisha saratani, kuharibu maini, mfumo wa kinga, kusababisha tatizo la tezi la shingo na matatizo mengine ya mfumo wa mwili wa binadamu.

**ITAENDELEA**

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Baada ya corona kutishia kambi za taaluma mkoa waibuka kivingine



Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka (katikati), akiwa na baadhi ya wanafunzi wa kike wa Shule ya Sekondari Bariadi, baada ya kufunguza kikao kazi cha viongozi na watendaji wa idara ya elimu, kilicholenga kuweka mikakati ya kuimarisha taaluma mkoani humo, Machi, mwaka jana. **PICHA: MTANDAO**

WAKATI huu ambao shule zimefungwa ili kuepusha wanafunzi na maambukizo ya virusi vya corona, mikakati mbalimbali inafanyika ili kuhakikisha wanaendelea na masomo wakiwa nyumbani.

Simiyu ni miongoni mwa mikoa ambayo imebuni mikakati ya kusaidia wanafunzi wake kujiandaa ya mitihani iliyo mbele yao, hasa wa darasa la nne, la saba, kidato cha nne na cha sita.

Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka, anasema, wiki iliyopita katika mahojiano na Nipashe kuwa Simiyu ilizindua mkakati huo ambao utasaidia wanafunzi mkoani humo kupokea masomo kawaida kupitia mitandao ya kijami, viongozi na redio.

"Tumezindua mkakati wa wanafunzi wetu kusoma wakiwa kwenye likizo hii ya ugonjwa wa Covid 19, pamoja na changamoto za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) kwenye baadhi ya maeneo yetu ya mkoa. Wakuu wetu wa shule, walimu wakuu na walimu wa masomo kupitia group la whats app, wameendelea kutoa kazi za kimasomo, kuprinti maswali na wanafunzi kuyapokea kupitia viongozi wa vijiji, vitongoji, maeneo ya ibada na redio," anasema Mtaka.

### WANACHOLENGA

Mkuu wa Mkoa anasema, malengo makuu ya mkakati huo ni kumwezesha mwanafunzi kuendelea kujifunza na pia walimu kuwa na mawasiliano ya kitaaluma na wanafunzi wao, wazazi kufanya ufuatiliaji wa kitaaluma kwa watoto wao.

> "Watoto wenyewe pia wanatakiwa kutulia nyumbani wakijisomea kipindi hiki cha likizo, pamoja na hayo, tahadhari zote za maambukizo ya virusi vya corona zimezingatiwa.

"Watoto wenyewe pia wanatakiwa kutulia nyumbani wakijisomea kipindi hiki cha likizo, pamoja na hayo, tahadhari zote za maambukizo ya virusi vya corona zimezingatiwa, anasema.

Mkuu huyo wa mkoa anafafanua kuwa shule zitakapofunguliwa, wanafunzi wa madarasa ya mitihani ya taifa kuanzia darasa la nne, la saba, kidato cha nne na cha sita, watapewa mitihani maalum ili kuwapima.

"Lengo la kuwapima mara baada ya shule kufunguliwa, ni kutaka ili kujua ni kiasi gani wamefanya na kuelewa yale, ambayo walipokea wakati wakiwa likizo ya corona," anasema.

### MKOA KIHISTORIA

Mkoa wa Simiyu chini ya Mkuu wa Mkoa Mtaka ndiyo mwanzilishi wa kambi za kitaaluma nchini, tangu Julai mwaka 2016 na sasa baadhi ya mikoa imeanza kuiga ubunifu huo ambao umechangia kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Simiyu ilibuni kambi hizo na bado inaendelea nazo ingawa mwaka huu zimekwama kufanyika kutokana tishio la maambukizo ya virusi vya corona ambalo limesababisha shule kufungwa.

Hatua ya serikali kufunga shule ni kuepusha msongamano wa wanafunzi, ambao unaweza kusababisha kuenea kwa virusi hivyo, kwa hiyo hata kambi za kitaaluma zimekwama kuendelea kutokana na hilo. Baada ya kukwama kuweka kambi hizo, mkoa umeamua kuja na mkakati huo mpya kwa wanafunzi ili kuhakikisha kwamba likizo hiyo ya dharura haiendi bure na badala yake inakuwa ni mbadala wa kambi za kitaaluma.

### MAFANIKIO

Katika matokeo ya kidato cha nne kwa mwaka 2017, inaelezwa kuwa ufaulu ulikuwa ni asilimia 70.68 na kisha mwaka 2019, ufaulu huo uliendelea kupanda hadi kufikia asilimia 86.46.

Pamoja na hayo, inaelezwa kuwa kwa miaka miwili mfululizo kuanzia 2018 na 2019 mkoa huo umekuwa miongoni mwa mikoa 10 bora katika matokeo ya kidato cha nne na kidato cha sita.

Hiyo ilikuwa ni taarifa iliyosomwa na Ofisa Elimu wa Mkoa wa Simiyu, Ernest Hinju mbele ya mgeni rasmi, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu, Stella Ikupa.

Aliweka wazi kuwa mkoa huo umeendelea kufanya vizuri kwa miaka ya hivi karibuni kuanzia mwaka 2017, ukiwa na shule nyingi za serikali ambazo ni za kata, huku za binafsi zikiwa chache, tofauti na mikoa mingine nchini.

Kwamba mkoa wa Simiyu una shule za msingi za serikali 529, wakati za watu binafsi zikiwa ni 10, huku shule za sekondari za serikali ambazo ni za kata zikiwa ni 144, na za binafsi 11.

Naye naibu waziri, katika hotuba yake wakati wa kufunga rasmi kambi za kitaaluma mkoani, aliwapongeza viongozi wa mkoa wakiongozwa na mkuu wa mkoa huo, Anthony Mtaka kwa ubunifu huo.

Ikupa alifunga kambi hizo Oktoba mwaka jana na kushauri watu wengine kuiga ubunifu huo wa mkoa wa Simiyu ili kusaidia kuinua kiwango cha taaluma kwa wanafunzi nchini.

"Nampongeza mkuu wa mkoa kwa ubunifu mkubwa wa kuandaa kambi hizi kwani, naamini wanafunzi mmejifunza mambo mengi na mtafanya vizuri katika mtihani wenu, ningeshauri watu wengine waige jambo hili," alisema Ikupa.

Aliongeza kuwa serikali imeendelea kuboresha sekta ya elimu nchini kwa kuongeza bajeti katika shule, kujenga madarasa, na anaamini itaendelea kutatua changamoto ya walimu mkoani Simiyu, na nchini kwa ujumla.

### CHANGAMOTO

Inaelezwa kuwa mwazoni wakati mkuu huyo wa mkoa anatoa wazo la kuazishwa kwa kambi za taaluma kulikuwa na changamoto zikiwamo za ukosefu wa mahitaji muhimu ya wanafunzi wa kike.

"Hilo halikutukatisha tamaa, na tulianza na wanafunzi wa kidato cha sita tu tena kwa muda wa wiki mbili, kwa sababu ya changamoto, lakini kadri miaka inavyokwenda ndivyo zinazidi kupata umaarufu," anasema.

Anasema, wadau wa elimu hawakukata tamaa, na kwamba mwaka 2018 walikweka tena wanafunzi kambini kwa muda wa mwezi mmoja huku hali ikianza kubadilika kufuatia mkoa kushika nafasi ya 10 kwa mara kwanza.

"Baada ya matokeo hayo, hata wanafunzi wa kidato cha nne mwaka uliofuata wa 2018 nao walikwekwa kambini kwa muda wa siku 30 na hivyo kambi hizo zikawa ni ajenda ya mkoa hadi leo," anasema.

Mtaka anasema, mwaka huu kambi za kitaaluma zimekwamishwa na tishio la virusi vya corona, lakini wakaamua kuja na mkakati mwingine wa kuhakikisha wanafunzi wa mkoa huo wanaendelea kufanya vizuri.

Mkakati: Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka (wa pili kushoto) akiwa na viongozi wengine wa mkoa huo wakati wa kuzindua mkakati wa kusoma kipindi cha likizo ya tahadhari ya corona.

Mkakati 2: Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka (katikati), akiwa na baadhi ya wanafunzi wa kike wa Shule ya Sekondari Bariadi, baada ya kufunga kikao kazi cha viongozi na watendaji wa idara ya elimu, Machi mwaka jana, kilicholenga kuweka mikakati ya kuimarisha taaluma mkoani humo.

ELIMU

**NA SHAMSI VUAI NAHODHA, ZANZIBAR**



Vifaa vya teknolojia ya kisasa kama 'satilaiti' vyenye uwezo wa kusafiri anga za juu, ni moja ya kazi za binadamu zinazoakisi mafanikio kiugunduzi, lakini tishio la kuangamizwa na virusi linabakia kuwa changamoto isiyojibika. **PICHA: MTANDAO**

# Janga la corona na tafakuri ya uwezo, ukuu wa Mungu

MWENYEZI Mungu anaporuhusu balaa na mitihani ya maisha, anawapa watu wenye hekima muda wa kutafakari uwapo na uwezo wake na makosa wanayoyafanya katika mazingira wanayoishi.

Kwa hulka yake binadamu ni kiumbe mwenye kiburi sana hasa anapokuwa na uwezo mkubwa wa elimu, mali na siha au afya.

Binadamu anapokuwa na uwezo huo anafikiri anajua kila jambo na hakuna litakalomshinda hapa duniani. Kwa bahati mbaya kuzuka kwa ugonjwa wa corona kunampa binadamu uzoefu mpya na uwezo wa kutafakari juu ya uwezo wake wa kujua mambo.

Wanasayansi wa tiba waliobobea wanakiri kwamba ugonjwa wa corona ni mpya na hawaufahamu vya kutosha. Ukweli huu umethibitisha kwamba uwezo wa bindamu una kikomo kinyume alivyokuwa akijua mwanzo.

Binadamu wanapaswa kujua kwamba mwanzo wa mwisho wa uwezo wake ndipo unapoanza ukuu na uwezo wa Mwenyezi Mungu muumba wa kila kitu.

Viongozi wa kisiasa wanaoongoza mataifa wanapaswa kuujua ukweli huu iwapo wanataka kufanikiwa katika kupambana kikamilifu na ugonjwa wa corona.

Hapana shaka Rais John Magufuli amekuwa kiongozi wa kwanza duniani kutambua kwamba Watanzania wanapaswa kufuata maagizo yote ya wataalamu na wanasayansi ya tiba ili kupambana na ugonjwa wa corona. Lakini, wakati wakifanya hivyo wasimsahau Muumba wao.

Japo inasikitisha sana tunapowasikia baadhi ya watu wakidharau msimamo huo.

Watu hawa wanasema si busara kuacha njia za sayansi za kupambana na corona na badala yake tukakimbilia kwa Mungu.

Watu wanaofikiri hivyo wanasahau kuwa hiyo sayansi wanayoizungumzia inatoka katika vitabu vitakatifu. Ukisoma kwa makini vitabu hivi utaona mambo matatu.

> Kwa bahati mbaya Waafrika waliziacha dawa hizi baada ya kuja wakoloni ambao hawakupenda tuendelee na dawa hizi kwa kisingizio cha kukosa ubora na vipimo vya kisayansi.

Mambo haya ni sayansi, falsafa ya maisha na utukufu wa Mwenyezi Mungu. Hawa wanasayansi tunawaowajua na tusiowajua wote wameumbwa na Mungu na kuipata elimu yao kwenye vitabu vitakatifu.

Nitatoa mfano mmoja wa mtaalamu wa tiba anayeitwa Ibin Sina aliyepata utaalamu wa tiba ya binadamu kutoka kwenye kitabu kitakatifu.

Ubingwa wake umenakiliwa sana katika " Canon of Medicine na kutumika duniani kote hata sasa.

Watu wengi hawafahamu kuwa haya mambo yanayosisitizwa na wanasayansi kuhusu namna ya kupambana na corona - usafi wa nguo na mwili, kuacha kukumbatiana au kubusiana yanatoka kwenye vitabu hivyo.

Katika dini mitume wanasisitiza usafi, kwa hiyo waamini wanapaswa kujisafisha kikamilifu.

Kwa upande mwingine vitabu hivyo vinasema jisafisheni na acheni mambo yenu maovu.

Watu wanaokosoa na kudharau kauli ya Rais Magufuli kuhusu kuheshimu maagizo ya wataalamu na kumtanguliza Mungu katika mapambano yetu dhidi ya corona wanaupata wapi ujasiri huo?

Inaonyesha ama hawajui hiyo sayansi wanayoizungumgumza au hawajui uwezo wa Mungu. Rais Magufuli ni mtaalamu wa kemia wa kiwango cha juu sana.

Kama tunavyoelewa taaluma ya kemia hasa " biochemistry " ina uhusiano wa karibu na biomedical science. Kwa mnasaba huu mtaalamu wa kiwango hiki anajua uwezo na ukomo wa sayansi .

Ikiwa mwanafunzi Chuo kikuu cha Dar es Salaam na Uingereza alifanya majaribio mengi ya kisayansi kwenye maabara.

Kwa hiyo anatambua vizuri sana ukomo wa akili ya mwanadamu katika kujua mambo ya kisayansi.

Rais Magufuli anachokisema ni ukweli mtupu. Hapana shaka ukweli huu unawaumiza baadhi ya watu. Hawapendi jinsi alivyokuwa na maono na upeo wa kujua mambo.

Anaona mambo ambayo viongozi wengi wa Afrika hawayaoni. Hili si jambo la kushangaza.

Mara nyingi viongozi wenye maono makubwa wanaposema mambo yanapuuzwa na kuonekana hayafai. Hali hii inatokea kwa sababu wanazumgumzia mambo ambayo yana upeo wa mbali.

Mfano mujarabu ni wa jambo hili mtaalamu wa Jiografia Galilee alipuuzwa aliposema dunia ni duara. Lakini leo inethibitika. Mwalimu Julius Nyerere na Kwame Nkurumah pia mawazo yao yalipuuzwa wakati wa uongozi wao .

Watu wengi wamefahamu falsafa na maono ya Mwalimu na Nkurumah baada ya viongozi hawa kufariki dunia.

Pili, kuzuka kwa ugonjwa wa corona kunatupa nafasi ya kutambua umuhimu wa tiba na vyakula vya asili.

Hivi sasa wataalamu wa lishe na tiba asili wanathibitisha ubora wa vyakula asili hasa machungwa, malimau, tangawizi na binzari katika kujenga kina ya mwili.

Vyakula hivi viliwasaidia sana wazee wetu kujikinga na kupambana na maradhi.

Vile vile dawa zetu za asili zimeonyesha zina uwezo wa mkubwa wa kutibu maradhi kadhaa.

Wazee wetu walizitumia dawa hizi kwa miaka mingi sana.

Kwa bahati mbaya Waafrika waliziacha dawa hizi baada ya kuja wakoloni ambao hawakupenda tuendelee na dawa hizi kwa kisingizio cha kukosa ubora na vipimo vya kisayansi.

Inawezekana sana dawa hizi hazikuwa na vipimo. Lakini hatuwezi kuziacha bila ya kuzifanyia utafiti.

Kwa vyovyote itakavyokuwa, umefika wakati kwa vyuo vikuu vyetu , taasisi ya utafiti wa dawa na tiba NIMR na kitengo cha tiba asili Chuo Kikuu cha Sayansi za Tiba Muhimbili (Muhas) kufanya utafiti wa dawa zetu.

Wapo wataalamu wa tiba asili wanaosema kuwa mmea wa kivumbasi unaweza kutibu mgonjwa yanayosababishwa na virusi.

Wakati wanasayansi wa Ulaya, Asia na Marekani wanafanya utafiti wa dawa ya corona, wataalamu wetu nao waanze kuutafiti mmea wa kivumbasi ili kujua kwa kiasi gani unaweza kutibu corona. Nina hakika tutafanikiwa kupata dawa mapema kuliko Ulaya.

Wataalamu wetu wakumbuke maneno ya vitabu vitakatifu "watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa". Ili tusiangamie tunapaswa tuyatafute maarifa haya kutoka kwa tiba za mababu zetu.

***Mwandishi ni Waziri Kiongozi mstaafu na Mbunge wa Kijitoupele Zanzibar.***

UCHAMBUZI

NA REUBENI LUMBAGALA

# Mapinduzi elimu yanautegemea mkopo huu wa Benki ya Dunia



Miundombinu kama madarasa, vyoo na maabara ni muhimu kwenye kuboresha elimu. **PICHA: MTANDAO**

SEKTA ya elimu ni muhimu katika maendeleo ya nchi ili kuiendeleza na kuikuza. Upatikanaji wa fedha ni nyenzo muhimu inayowezesha kupanga mipango na mikakati ambayo itaboresha sekta hiyo kikamilifu.

Serikali ndiyo yenye dhamana ya kukuza sekta zote na kuleta maendeleo huku elimu ikipewa kipaumbele. Ndiyo maana serikali inafanya juhudi ili kufanikiwa katika mipango na mikakati ya kuleta maendeleo yanayogusa na kuboresha maisha ya watu kupitia elimu.

Hata hivyo, ni vigumu kwa serikali kufanikisha mipango yake bila fedha au misaada kutoka sekta binafsi. Ndiyo maana serikali inasisitiza ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi (Public and Private Partnership) katika shughuli za kimaendeleo.

Taasisi za fedha mathalani benki za ndani na nje ni wadau muhimu katika maendeleo ya elimu nchini kupitia misaada na mikopo wanayoitoa ili kufikia malengo yaliyowekwa kwa sekta ya elimu.

Taasisi za fedha zinatoa misaada ya rasilimali fedha na vitu kama viti, meza, madawati, vitabu, kompyuta, madaftari ili kusaidia juhudi za kuinua sekta ya elimu.

Benki ya Dunia (WB) imekua ikitoa mikopo kwa nchi mbalimbali duniani katika kuchagiza maendeleo ya elimu.

Tanzania kama yalivyo mataifa mengine iliamua kukopa mkopo wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa mradi wa kuboresha elimu ya sekondari (SEQUIP) ili kuweka mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari nchini. Mradi huu unategemewa kunufaisha wanafunzi 6,000,000, hivyo ni vyema kuangalia namna ambavyo taifa litafaidika.

> “Watoto wa kike wamekuwa wakipata vikwazo kutokana na umbali wa shule na kusababisha kupata changamoto wanapokwenda ama kurudi shuleni kwa hiyo kupitia mradi huu, tunakwenda kujenga shule za bweni kwa ajili ya watoto wa kike.



### TIJA YA MKOPO

Namba moja itakuwa kujenga miundombinu ya shule, lengo likiwa ni utekelezaji wa sera ya elimumsingi bila ada ambao umezalisha changamoto ya mahitaji ya miundombinu kama vile madarasa, ofisi za elimu, vyoo na nyumba za walimu.

Hii ni kutokana na ongezeko la wanafunzi katika shule za sekondari. Hivyo, kupitia mkopo huu, serikali inakusudia kujenga shule nyingi ili kuwezesha wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri kwa kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

“Serikali imefanya jitihada kubwa ya kuongeza miundombinu katika maeneo mbalimbali ya elimu baada ya mwitikio mzuri wa elimu bila ada, ambao utaongeza idadi kubwa ya wanafunzi wanaokwenda kujiunga na elimu ya sekondari. Mradi huu utasaidia katika kuboresha na kuongeza miundombinu katika shule za sekondari nchini ambazo zitapokea wanafunzi hao waliotokana na mwitikio wa elimu bila malipo,” anasema Profesa Ndalichako.

Pili ni kuimarisha utoaji wa ushauri nasaha ili wanafunzi wanaotoka familia zenye changamoto mbalimbali za kijamii ama mazingira duni wawe na mahali pa kusemea ili serikali ichukue hatua stahili kwa ustawi bora wa wanafunzi hao.

Pasipo kuwatambua wanafunzi wanaotoka mazingira magumu na utoaji wa ushauri nasaha, baadhi yao watashindwa kuendelea na masomo na hivyo kushindwa kutimiza ndoto zao wanazotaka kuzifikia katika maisha yao ya baadaye.

Tatu, kutoa mafunzo kazini kwa walimu yakiwamo ya kidijitali kwa wanafunzi. Mafunzo kazini pia ni muhimu katika kuhakikisha walimu wanaendana na kasi ya maendeleo iliyopo.

Miongoni mwa mipango ya Wizara ya Elimu ni kuwapatia walimu mafunzo ili kuongeza ujuzi na stadi ili kufundisha wanafunzi kisasa zaidi kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Aidha, wanafunzi wanapata mafunzo ya digitali katika ujifunzaji. Hii ni kutokana na umuhimu wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) katika kufundisha na kujifunza.

Kupitia Tehama, walimu na wanafunzi watapata maarifa na stadi mbalimbali kupitia elimu ya mtandaoni.

Aidha, suala jinginge muhimu la nne ni kuwaboreshea wanafunzi wa kike mazingira ya kujifunza. Mradi huu umekusudia kuwapunguzia changamoto wanawake wanaokabiliwa na changamoto ya kutembea umbali mrefu kwenda shule, hali inayohatarisha usalama wao.

Miongoni mwa maeneo ambayo fedha za mkopo huu zitaelekezwa ni katika ujenzi wa mabweni kwa ajili ya wasichana.

“Watoto wa kike wamekuwa wakipata vikwazo kutokana na umbali wa shule na kusababisha kupata changamoto wanapokwenda ama kurudi shuleni kwa hiyo kupitia mradi huu, tunakwenda kujenga shule za bweni kwa ajili ya watoto wa kike,” anasisitiza Waziri wa Elimu Ndalichako.

Pia mradi utajenga shule mpya maalum za wasichana zenye mabweni.

Kwa hakika, mkopo huu una tija kubwa kwa taifa hili kwani unakwenda kuwanufaisha watoto ambao baadhi yao wanatoka kwenye kaya maskini.

Kutokana na uboreshwaji wa sekta ya elimu kupitia mkopo huu, watoto kutoka kaya maskini wanatarajiwa kupata elimu bora kutokana na fedha kuelekezwa kwenye uboreshaji wa mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji.

Kwa hiyo ni vyema wazazi na walezi waendelee kuwalinda na kuwakinga watoto wao wakati huu wa likizo ya corona ili wawe na afya njema na kunufaika na mkopo huu wa elimu kutoka Benki ya Dunia.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***



# Shekhe ahimiza uvaaji barakoa kwenye misikiti

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

SHEKHE wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata), Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, amewataka waumini kuvaa barakoa wanapoingia kwenye misikiti ili kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa corona.

Shekhe Rajabu alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki alipokuwa akitoa nasaha zake kwenye Msikiti Mkuu wa Gadafi jijini hapa.

Alisema wanapaswa kuvaa barakoa kama wanavyovaa kofia za baragashia ili kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huo.

Pia aliwasisitiza kuvaa barakoa kwenye maeneo yenye mikusanyiko ya watu kama vituo vya mabasi na sokoni.

"Ili kutekeleza azma ya kila mtu kuvaa barakoa inapaswa kuzingatiwa na kila muumini kwa kuwa itasaidia kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huu, na kwa pamoja tutaweza kuutokomeza kwa kufuata maelekezo kutoka kwa waatalamu wa afya, viongozi wa serikali na madhehebu ya dini kama wanavyotoa elimu ya jinsi ya kujikinga.

"Ugonjwa huu ni wa hatari hivyo ninawaomba waumini wote wa dini ya Kiislamu kuhakikisha wanapoingia misikitini na maeneo mengine mnajihadhari kwa kuvaa barakoa, kunawa kwenye maji yanayochuruzika na sabuni ili kujilinda na janga hili la corona," alisema.

Aliwasisitiza waumini kufuata maelekezo yaliyowekwa ndani ya misikitini ikiwamo kukaa kwa umbali na kutosalimiana kwa mikono.

"Haya tunayowaeleza pia mnapaswa kuyafuata mkiwa majumbani zingatieni kanuni za kujilinda na janga hili kwenye familia kwa kuweka vifaa vya kama madumu ya maji na sabuni," aliwashauri.

Aidha, alieleza kuwa ugonjwa huo utatoweka kama kila Mtanzania atafuata maagizo ya wataalamu wa afya na kuondoa hofu.

"Pia tukiondoa tofauti za itikadi za dini na kuungana kumuomba Mwenyezi Mungu, hapo tutaweza kushinda janga hili la corona," alisema.

Hata hivyo, aliwataka waumini hao kufanya kazi kwa bidii ili kujipatia kipato na kuishi kwenye misingi ya kumpendeza Mungu.

**"Ugonjwa huu ni wa hatari hivyo ninawaomba waumini wote wa dini ya Kiislamu kuhakikisha wanapoingia misikitini na maeneo mengine mnajihadhari kwa kuvaa barakoa, kunawa kwenye maji yanayochuruzika na sabuni ili kujilinda na janga hili la corona," alisema.**

# Mahabusi, wafungwa wapewa vifaa kinga maambukizo corona

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

JESHI la Magereza limepokea msaada wa vifaa mbalimbali kwa ajili ya mahabusi na wafungwa wa Gereza Kuu la Isanga, kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Vifaa hivyo vimetolewa na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Anthony Mavunde na Mtandao wa Watumishi wa Umma Wanawake ujulikanao kama Viongozi Wanawake Wanaoibukia Tanzania (EWLT).

Akipokea msaada huo jana, Kamishna wa Magereza nchini, Suleiman Mzee, aliwashukuru wadau hao kwa kulisaidia jeshi hilo kukabiliana na ugonjwa huo.

"Mavunde nikushukuru sana kwa msaada wa vifaa hivi ulivyovikabidhi leo katika Gereza Kuu la Isanga, Dodoma kwani vitasaidia maofisa, askari pamoja na wafungwa na mahabusi katika kujikinga na corona magerezani," alisema.

Alisema jeshi hilo limeendelea kuchukua hatua za tahadhari ikiwamo kusitisha kwa huduma zote za kutembelea wafungwa na mahabusi ikiwa ni pamoja na upelekaji wa vyakula kwa mahabusi waliopo magerezani.

Aidha, alisisitiza kuwa jeshi hilo pia linachukua tahadhari na hatua kwa kadri litakavyoona inafaa sambamba na kuzingatia miongozo mbalimbali inayotolewa na serikali dhidi ya kujikinga na maambuzo ya ugonjwa huo.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Mavunde alisema magereza ni eneo ambalo linapaswa kusaidiwa vifaa kama vile ndoo za kunawia mikono, sabuni na vitakasa mikono ili kujikinga na ugonjwa huo.

"Msaada huu ni mwanzo tu, lakini nitaendelea kutoa msaada pale gereza hili litakapohitaji ili kupambana na ugonjwa wa corona usiingie gerezani," alisema.

Katika hatua nyingine, jeshi hilo lilipokea msaada wa vifaa mbalimbali vya kibinadamu kwa ajili ya wafungwa na mahabusi vyenye thamani ya Sh. milioni 5.5 ambavyo vimetolewa na mtandao wa EWLT.




Fatuma Ramadhani mjane (kushoto), akipokea msaada wa vyakula kutoka kwa Sheikh wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata), Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu (wa pili kulia), vilivyotolewa na Meneja wa Taasisi ya Dar-ul- Muslimeen, Musilimu Banji (kulia) kwa wajane na yatima wa Kata ya Changombe, jijini Dodoma jana, kwa ajili ya mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Wa tatu kulia ni Mbunge wa Viti Maalumu, Mariamu Ditopile. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Tarura yahitaji bil. 127/- kurejesha barabara zilizoharibiwa na mvua

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesema Sh. bilioni 127 zinahitajika ili kurejesha miundombinu ya barabara ambazo zinasimamiwa na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura), zilizoharibiwa na mvua mwaka huu.

Jafo alitoa kauli hiyo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumzia hali ya barabara hizo na uharibifu uliopo.

Alisema Tarura imefanya tathmini ya barabara zote zilizoharibika ambapo inahitajika Sh. bilioni 127 kuzirejesha kwenye hali yake.

"Nawaomba Watanzania tuwe na subira kipindi hiki ambacho kuna changamoto kubwa, tujue kwamba kwa sasa barabara zimeanza kurejeshwa ingawa ni fedha nyingi zinahitajika," alisema.

Alieleza kuwa serikali kupitia Tarura ilifanya uwekezaji mkubwa wa miundombinu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na ziliboreshwa kwa kiwango kikubwa.

"Hata hivyo mvua zilizonyesha mwaka huu, miundombinu iliharibika kwa kiwango kikubwa, sio tu inayosimamiwa na Tarura peke yake, hata inayosimamiwa na Tanroads (Wakala wa Barabara Tanzania)," alisema.

Waziri Jafo alisema mvua kwa mwaka huu ilikuwa kubwa na miundombinu kwa kiwango kikubwa imeharibika sana.

"Niwashukuru wataalamu wa Tarura wamefanya tathmini ya barabara zote, Watanzania wafahamu kiasi hicho kinahitajika ili kurejesha miundombinu hiyo," alisema.

Aidha, alisema ujenzi wa barabara kwa ujumla wake hauwezi kufanyika wakati wa mvua zinanyesha, na kwamba wataalamu wameanza kurekebisha maeneo mengine kadri inavyowezekana.

"Kuna maeneo yaliyojaa maji kabisa inasubiriwa kidogo hali iweze kutengemaa ili baadaye maeneo hayo yarejeshwe vizuri, mwishoni mwa mvua hizi Tarura itahakikisha miundombinu yote inarejeshwa kwenye hali nzuri ili Watanzania wasafiri kutoka eneo moja hadi jingine na kutengeneza uchumi wa Taifa letu," alisema.

Aliongeza: "Nishukuru timu yangu ya Tarura nikiwa mimi msimamizi mkuu, vijana wangu wanafanya kazi kubwa sana huko site, ingawa sehemu nyingine mvua zimekuwa nyingi hata mitambo haiwezi kupita."

Alisisitiza kuwa anaamini mvua zinapoelekea ukingoni maeneo mbalimbali yataanza kurekebishwa taratibu kulingana na kipaumbele cha eneo husika.





## Tari kukutanisha wakulima mikoa Nyanda Juu Kusini

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (Tari) Uyole ya jijini Mbeya, imesema ina mpango wa kuimarisha kilimo kwa kuwakutanisha wakulima wa maeneo mbalimbali ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na kuwapa mbinu za kilimo bora pamoja na teknolojia za kisasa za uzalishaji.

Wakulima hao watafundishwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara yakiwamo mahindi, maharage, viazi mviringo, vitamu na lishe, ngano na maparachichi, lengo likitajwa ni kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Akizungumza na Nipashe Mkurugenzi wa Tari- Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema wameamua kuanza kupeleka teknolojia hizo kwa wakulima ili kuwezesha azma ya serikali ya kufikia uchumi wa kati.

Alisema awali walikuwa wanatoa elimu na teknolojia kwa wakulima baada ya mavuno, lakini wakabaini kuwa mfumo huo hauna tija kutokana na teknolojia hizo kutowafikia wakulima kwa ufasaha na hivyo wakaona ni vema waanze kuwafuata mashambani.

Dk. Bucheyeki alisema baada ya kufanya utafiti, walibaini wakulima wanashindwa kuzichukua teknolojia wanazofundishwa kwa sababu hazielezewi thamani yake kwa mfumo wa fedha, hivyo wakaona ni bora wawaeleze wakulima kuwa akilima na kupanda kwa kutumia teknolojia hizo watapata fedha kiasi fulani.

"Tutaanza na wakulima pamoja na vikundi vyao kuwaeleza kwamba wakilima mahindi, ngano, maharage, viazi na soya na kwa kutumia mbegu zinazozalishwa na watafiti watapata kiasi fulani cha fedha kwa eneo ili wahamasike zaidi," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisisitiza kuwa kituo hicho kinazalisha mbegu kulingana na hali ya hewa na mazingira ya eneo ambalo mbegu hizo zinapandwa ili kuwarahisishia wakulima.

Ofisa Kilimo Mtafiti wa Tari-Uyole anayeshughulikia mahindi, Boniface Minja, alisema mafunzo ya kilimo ni muhimu kwa wakulima kutokana na mahitaji ya serikali ya kufikia uchumi wa viwanda ambao unahitaji malighafi za kutosha na zenye ubora.

Alisema teknolojia wanazofundishwa wakulima ni kwa ajili ya kuongeza tija kwenye mazao wanayozalisha iii chakula kipatikane kwa wingi na malighafi kwa ajili ya viwanda zipatikane.

Minja alisema wakulima wengi wanakosea kwenye uzalishaji kwa kutumia teknolojia zilizopitwa na wakati hali inayowafanya wasipate tija inayotarajiwa, hivyo akawashauri wazingatie teknolojia mpya wanazofundishwa.

Mmoja wa wakulima, Gwamaka Mwaipyana, alisema tumeanza kuzitumia mbinu walizofundishwa ili kuongeza tija kwenye kilimo chao kwa maelezo kuwa kilimo cha mazoea kimekuwa kikiwaumiza.

# Wazee wa mila waonya familia kuoza watoto kipindi cha corona

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

WAZEE wa kimila wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wamezionya familia ambazo zinatumia ugonjwa wa Covid-19 kuwa sababu ya kuwaozesha watoto.

Akizungumza mwishoni mwa wiki walipokuwa wakifanya tambiko kwenye msitu uliopo katika Kitongoji cha Mlimani mjini Rujewa, Katibu wa mila wa kabila la Wasangu, Mwanasimtwa Mwagongo, alisema kipindi hiki cha janga la corona kinapaswa kuchukuliwa tahadhari zote zinazotolewa na wataalamu wa afya badala ya kuwa daraja la kufanikisha mipango ya kuozesha watoto ambao wako likizo.

Mwagongo alisema mapambano dhidi ya Covid-19 yanahitaji nguvu ya pamoja kwa kuhakikisha hakuna mtu anayeachwa nyuma, hivyo kitendo cha baadhi ya familia kuona kama fursa ya kuozesha au kuwapa mimba watoto sio jambo la kiungwana linapaswa lishughulikiwe.

"Wazee wa mila Mbarali, tumeamua kuunga mkono juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya corona kwa kumuomba Mungu wetu atuepusha... lakini kuikumbusha jamii kuchukua tahadhari zote muhimu ili janga hili lipite, na shughuli zirejee kama ilivyokuwa awali, hatufurahishwi kusikia mabinti wanapata mimba mara wanaolewa," alisema Mwagongo.

Alisema wakati huu ambapo shule zimefungwa, wazazi wanapaswa kuwa waangalifu kwa watoto wao kwa maelezo kuwa itasaidia kuepukana na vishawishi kutoka kwa mafataki ambao kazi yao ni kuharibu ndoto za mabinti.

Ofisa Afya wa Mkoa wa Mbeya, Mashaka Juma, aliwashukuru wazee wa mila kuunga mkono serikali katika vita dhidi ya corona kwa kutumia imani yao na kwamba anaamini Mungu atasikia maombi ya kila mmoja.

"Wazee wa kimila mmekuwa mstari wa mbele kwa kuhakikisha nchi inaendelea kuwa na amani na utulivu, lakini kuhamasisha matumizi ya dawa za asilia, tuna imani tutavuka salama dhidi ya janga hili," alisema Juma.



Mwendesha pikipiki maarufu 'bodadoda' akivunja sheria za usalama barabarani kwa kubeba abiria wawili maarufu 'mshikaki; katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, mkoani Mbeya, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wasindikaji Mbarali walia uzalishaji mdogo mpunga

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAMILIKI wa viwanda vya kusindika mpunga katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, wamesema kiwango cha mpunga kinachozalishwa na wakulima hakikidhi mahitaji ya viwanda vyao.

Wamelalamika kuwa hali hiyo inawakwaza kufanya kazi katika kipindi chote cha mwaka.

Mwenyekiti wa wamiliki wa viwanda vya kusindika mpunga Wilaya ya Mbarali, Venance Mgeni, alisema kiwanda cha aina yoyote kinahitaji kuwa uhakika wa malighafi, lakini viwanda vya mbarali vinategemea mpunga kama malighafi kutoka kwa wakulima wadogo, ambao nao hawazalishi kwa tija.

Pia alisema kuna mashamba mengi katika wilaya hiyo ambayo yanafaa kwa kilimo cha mpunga, lakini hayalimwi, na sababu za mashamba hayo kutolimwa hazifahamiki.

Mgeni aliiomba serikali kufanya sensa ya mashamba ili kubaini yasiyolimwa kuwagawia wamiliki wa viwanda ili na wao washiriki kuzalisha mpunga kwa ajili ya viwanda vyao.

"Tunaiomba serikali ifanye sensa ya mashamba kwa ajili ya kuainisha mashamba ambayo hayalimwi bila sababu za msingi na wakishajua wayagawe kwa wamiliki wa viwanda ili na wao wazalishe na kuwa na uhakika wa kupata malighafi za viwanda vyao," alisema Mgeni.

Alisema kutokana na uhaba wa malighafi, viwanda vingi vinafanya kazi kwa msimu kutokana na uhaba wa malighafi, hali ambayo inasababisha uendeshaji wa viwanda hivyo kuwa mgumu pamoja na kuwakosesha wananchi ajira zenye uhakika.


"Ukosefu wa mpunga wakutosha kwa ajili ya viwanda vyetu unasababisha tufanye kazi kwa msimu, sasa ule muda ambao tunafunga viwanda kwa kukosa malighafi tunalazimika kuzuia na ajira za baadhi ya wafanyakazi ili kuepuka kupata hasara," alisema Mgeni.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema kuwa mavuno ya mpunga katika msimu uliopita hayakuwa mazuri kutokana na uhaba wa mvua, ingawa mashamba yaliyolimwa yalivuka lengo la makisio ya halmashauri hiyo.

Mfune alisema katika makisio ya halmashauri hiyo ilikuwa kulima hekta 125,388 za mpunga na kuvuna tani 555,720, lakini kiwango hicho hakikufikiwa kutokana na mtawanyiko wa mvua katika wilaya hiyo kutokuwa mzuri kama walivyotarajia.

Alisema baadhi ya mashamba ya wilaya hiyo yanategemea kilimo cha umwagiliaji, lakini kutokana na mvua kutonyesha kwa kiwango kinachotakiwa mito nayo haikuwa na maji ya kutosha.

Aliwataka wamiliki wa viwanda kuwa na umoja na kushirikiana katika kutatua changamoto zinazowakabili kwenye uzalishaji wao na kwamba serikali itaendelea kushirikiana nao katika kutatua changamoto zao.





# Ugatuzi wapunguza vifo vya wajawazito

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

TANGU kuanza kutekeleza mpango wa ugatuzi  Zanzibar, mafanikio makubwa yamefikiwa ikiwamo ujenzi wa hospitali za vijijini, hivyo kupunguza vifo vya kinamama kutoka asilimia 55 hadi 41.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalumu za (SMZ), Haji Omar Kheir, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020-2021.

Alisema mpango wa ugatuzi ambao ulianza utekelezaji wake miaka mitatu iliyopita, umelenga katika sekta tatu ikiwamo elimu ya msingi, kilimo pamoja na afya ya msingi ya vituo vya afya vijijini.

Alisema mpango wa ugatuzi umefanikiwa kutekeleza na kusimamia jumla ya miradi 21 na kugharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.5.

Aliitaja miradi hiyo ikiwamo ujenzi wa madarasa 72 ya elimu ya msingi, hivyo kupunguza uhaba wa wanafunzi ambao walikuwa wakijisomea chini ya sakafu.

Aidha, alisema utekelezaji wa ugatuzi katika sekta ya elimu ya msingi umepiga hatua kubwa ambapo jumla ya matundu ya vyoo 133 yamejengwa, hivyo kupunguza tatizo la msongamano katika shule kwa wanafunzi kupata huduma za vyoo.

"Mheshimi Naibu Spika, huduma za ugatuzi katika sekta ya elimu ya msingi zimepata mafanikio makubwa kwa kujenga madarasa ya wanafunzi 72 pamoja na matundu ya vyoo 133, hivyo kupunguza usumbufu wa wanafunzi ikiwamo wa kike kupata huduma za vyoo," alisema.

Kheir alisema utekelezaji wa ugatuzi katika sekta ya afya ya msingi umepata mafanikio makubwa ambapo wajawazito na watoto wamekuwa wakivitumia vituo hivyo kwa kiwango kikubwa.

Alisema hatua hiyo imesaidia kupunguza vifo vya kinamama kutoka asilimia 55 hadi 41.

"Tumepata mafanikio makubwa katika sekta ya afya katika mpango wa ugatuzi ambapo sasa upimaji wa afya kwa wajawazito uelewa wake ni mkubwa sana, hivyo kusaidia kupunguza vifo kutoka asilimia 55  hadi 41," alisema.

Waziri huyo alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na juhudi zake za kuimarisha vikosi vya SMZ na kuvifanya kuwa na uwezo wa kutoa huduma za ulinzi na jamii.

Alieleza kuwa Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimepatiwa vifaa vya kisasa ikiwamo boti kwa ajili ya kufanya doria na kupambana na wahalifu wanaofanya biashara ya magendo.

"Tumefanya maboresho makubwa katika vikosi vya SMZ kwa kuvipatia nyenzo za ulinzi na kuwa majeshi yenye uwezo wa kupambana na adui, na kuwa tayari kusaidia huduma za jamii," alisema.

# Sheria mpya yawataka Diaspora kuyatambua Mapinduzi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SHERIA mpya ya Jumuiya ya Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi (Diaspora) iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi, sasa inawataka jamii hiyo kuyatambua Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 kama ni moja ya tunu ya kitaifa na kielelezo cha Wazanzibari kuwa huru katika nchi yao.

Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda, Hassan Khamis Hafidh, alisema hayo wakati akichangia bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2020-2021, ambayo ndiyo yenye jukumu la Diaspora.

Alisema Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 ndicho kielelezo cha utu wa Mzanzibari kuwa huru katika nchi yake baada ya kuung'oa utawala wa kisultani.

Alieleza kuwa hicho ni kigezo muhimu ambacho jamii ya Diaspora wanatakiwa kukifahamu na kukitambuwa pamoja na kukiheshimu kama ni moja ya uzalendo wa kila Mzanzibari.

"Tumepitisha sheria ya Diaspora ambayo miongoni mwa masharti yake makubwa ni jamii hiyo kuyatambuwa Mapinduzi ya Januari 12, mwaka 1964 ambayo ndicho kielelezo cha utu na uhuru wa kila Mzanzibari kutoka katika utawala wa kisultani," alisema Hafidh, ambaye ni mwanzilishi wa Diaspora Zanzibar.

Akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2020-2021, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Issa Haji Ussi, alisema miongoni mwa masharti ya jamii ya Diaspora wanayotakiwa kuyazingatia ni kwamba hawataruhusiwa kushiriki katika harakati za kisiasa.

Aidha, alisema Diaspora hawataruhusiwa kuwa wanachama wa vyama vya siasa pamoja na kutoshiriki katika uchaguzi mkuu wa kuwachagua viongozi wa kitaifa.

"Sheria mpya ya Diaspora tuliyoipitisha haitawaruhusu Diapora kushiriki katika siasa pamoja na kuwa wanachama na kupigakura katika uchaguzi mkuu," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha sheria ya Diaspora ambayo sasa inawatambua rasmi jamii hiyo, hivyo kushiriki katika harakati mbalimbali ikiwamo michango ya maendeleo.



Mchuuzi wa nyanya akiwaonyesha wateja waliofika kununua bidhaa hiyo katika soko la Ilala, jijini Dar es Salaam. Tenga moja la nyanya liliuzwa kwa bei ya 25,000/-. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# SMZ kuendelea kuthamini mchango wa serikali China

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema itaendelea kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China katika kuunga mkono maendeleo na ustawi wa wananchi wa Zanzibar.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Mohamed Aboud, alisema hayo wakati akipokea msaada wa vifaa vya kusaidia mapambano dhidi ya virusi vya corona, vilivyotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia ubalozi mdogo uliopo Zanzibar.

Aboud alisema msaada wa maboksi 225 yenye vifaa tofauti ikiwamo nguo za kinga kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wa corona umekuja wakati mwafaka, huku Zanzibar ikiwa katika mapambano hayo.

Alisema mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha inapunguza kasi ya maambukizo ya ugonjwa huo.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa msaada wake, ambao umekuja wakati sahihi, huku Zanzibar ikiwa katika mapambano ya kuondosha ugonjwa huo moja kwa moja, na kutoa nafasi kwa wananchi na sekta nyingine kufanya kazi," alisema.

Aidha, Aboud aliwataka wananchi kufuata masharti yaliyowekwa na Wizara ya Afya katika kupambana na ugonjwa huo ikiwamo kuvaa barakoa, pamoja na kusafisha mikono na kuepuka mikusanyiko isiyokuwa na lazima.

Naye Balozi mdogo wa China, aliyeko Zanzibar, Xie Xiaowu, alisema wataendelea kuisaidia Zanzibar katika nyanja mbalimbali kutokana na nchi mbili hizo kuwa na uhusiano wa kihistoria na wa kindugu.

Alisema China inafahamu athari kubwa za kiuchumi inazozipata nchi zilizoendelea ikiwamo Zanzibar, ambapo sekta mbalimbali zimeathirika.

"Tunafahamu maumivu makubwa inayozipata baadhi ya nchi za Bara la Afrika kutokana na ugonjwa wa corona...uchumi umeathirika vibaya katika sekta mbalimbali ukiwamo utalii," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Kamisheni ya Maafa Zanzibar,  Makame Khatib, alisema shehena ya msaada huo itatumika na kuwafikia walengwa wakiwamo wahudumu sekta ya afya wanaofanya kazi moja kwa moja kuwahudumia wagonjwa.

"Shehena ya vifaa vya huduma ya kinga kwa wagonjwa wa corona vitawafikia walengwa wote wakiwamo wahudumu wanaofanya kazi moja kwa moja kwa wagonjwa wa corona," aliongeza.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA OFFA YA KIWANJA NA MKATABA WA SHAMBA

**PASCHAL J. MALLYA** anatangaza kupotelewa na Offa ya Kiwanja Plot No. 60 Block F Tabata pamoja na Mkataba wa shamba.

Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi: KMR/RB/5735/2019.

157379

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Rehema Enock Ndapisi** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba T 125 DNK Toyota Premio. Chassis namba NZT2400023967. Injini namba INZA465291. Rangi ya gari Silver.

Taarifa RB. NO **IR/IR/RB/844/2020***

157380

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

YAH: SHAURI NAMBA 39 LA 2019

MATHIAS ZA NYUMBA ……………..MDAI

DHIDI YA

NATIONAL MICROFINANCE BANK PLC & 3 WENGINE ………….. MDAIWA

KWA 1. ABIUDI VICENT SHELUKINDO
2. SHABANI JUMA

MATHIAS ZAYUMBA amefungua shauri mbele ya baraza la ardhi na nyumba wilaya ya Tanga dhidi yako. Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 19/05/2020 saa 5 kamili asubuhi (11.00). Hivyo basi, unatakiwa kufika kwenye Baraza hili bila kukosa Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (w) Tanga.

AMRI hii imetolewa na kutiwa Saini Muhuri/Lakiri wa Baraza hili leo tarehe 06/05/2020.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
TANGA

157381

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA OFFA YA KIWANJA

KHAMIS MOHAMED MALUNDI AMBAYE NI MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU MOHAMED ABDALLAH MKAZI WA SHINYANGA

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFFA YA KIWANJA NAMBA 5 KITALU 'G' MJINI KATI MANISPAA YA SHINYANGA, AMBAYO ILIPOTEA MWAKA 2020 MAENEO YA MTAA WA MBOYE MJINI SHINYANGA

KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA KHAMIS MOHAMED MALUNDI KWA SIMU NAMBA 0677-186853

RB NAMBA SHY/RB/2020,
COTROL NAMBA 9910812617833

JACOB F. MWINUKA
AFISA ARDHI
SHINYANGA

157370

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ

MARCELLAH CHIKELEA KOMBA anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaj yenye namba za usajili MC 729 BZJ TVS KING. Chassis namba MD6M14PA0J4E19363. Engine namba AK4EJ4X24277.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/364647/2020.**

157373

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

HENRY HERMAN KASENGA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 776 ATK AINA YA TOYOTA CORONA.

KWA YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI: GEI/MBO/RB/68193/2020.

157371

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

LUCAS AMBROSE NAELEWA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 964 DKR TOYOTA PREMIO. Chassis namba AZT2405002331.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Control No: 9910812621744.

157374

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

RWABANGI LUTEGANYA anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 800 CDF – TVS 125.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: WMB/RB/471/2020.

157375

## KADI YA GARI IMEPOTEA

BONIFACE NDEGE KIRIGIA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NO ZA USAJILI T 104 AQB SHORT CHASSIS LAND CRUISER.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

ARU/ARU/366119/2020.

157376


***NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Iran yaua wanajeshi wake 19 jaribio kombora jipya

**TEHRAN,** Iran

WANAMAJI 19 wameuawa na wengine 15 kujeruhiwa katika tukio la ajali lililohusisha meli za kijeshi za Iran katika Ghuba ya Oman, Jeshi la Iran limesema.

Vyombo vya habari vya Iran, vilisema kwamba meli hiyo kwa jina Konarak ilishambuliwa na kombora jipya lililokuwa likijaribiwa na meli ya kijeshi ya Frigate Jamaran wakati wa zoezi la kijeshi siku ya Jumapili.

The Konarak ilishambuliwa na kombora jipya Jumapili mchana wakati wa zoezi la kijeshi katika maji ya Bandar-e Jask Kusini mwa Pwani kulingana na runinga ya taifa katika tovuti yake.

Wanamaji hao walisema kwamba meli hiyo ilivutwa hadi ufukweni na kwamba uchunguzi umeanza. **BBC**

## Pence ajitenga mfanyakazi Ikulu kupata corona

**NEWYORK,** Marekani

MAKAMU wa Rais wa Marekani, Mike Pence (pichani chini), ameamua kujitenga kwa muda kama tahadhari baada ya mfanyakazi mmoja wa Ikulu kuthibitishwa kuwa na maambukizo ya virusi vya Corona.

Ofisa katika utawala wa Trump, alisema kuwa Pence ameamua kujitenga kwa hiari kwa mujibu wa muongozo wa wataalamu wa afya licha ya kufanyiwa vipimo na kuonyesha kuwa hajaambukizwa virusi hivyo.

Uamuzi wake wa kujitenga unatokana na hatua iliyochukuliwa na wanasayansi watatu walioamua kufanya hivyo baada ya kukaribiana na mfanyakazi katika Ikulu aliyethibitishwa kuwa na virusi vya Corona.

Msemaji wake, Devin O'Malley alisema Pence ataendelea kufuata ushauri wa kitengo cha matibabu cha Ikulu na wala hayuko karantini.

Pence amekuwa nyumbani kwake tangu siku ya Ijumaa na hakuonekana katika mkutano wa Rais Donald Trump na viongozi wa jeshi uliofanyika siku ya Jumamosi katika Ikulu ya White House mjini Washington. **DW**



# Roboti inavyotumika kupunguza corona Rwanda

**KIGALI,** Rwanda

RWANDA imesema kuwa tayari inatumia roboti katika kuzuia maambukizo ya virusi vya corona kwenye vituo vya ugonjwa huo.

Hatua hii inakuja baada ya taifa hilo kulegeza masharti ya sheria ya kutotoka nyumbani.

Waziri wa Afya, Dk. Daniel Ngamije alisema, zitasaidia kufanya kazi za kuhudumia wagonjwa wa Covid19 zikisaidiana na wauguzi na madaktari.

"Roboti inaweza kuchukua sampuli za mgonjwa badala ya muuguzi. Kuna kazi nyingi ambazo roboti zinaweza kufanya kuhudumia wagonjwa wa covid19, siyo kwamba wauguzi ama madaktari wameshindwa la hasha, ni kama kuwasaidia kupumua na pengine kuwapa nafasi kufanya mambo mengine ya kuwahudumia wagonjwa ipasavyo."

**Roboti inaweza kuchukua sampuli za mgonjwa badala ya muuguzi.**

Roboti hizo ambazo zimepewa majina ya Kinyarwanda zinatarajiwa kusaidia katika huduma zinazotolewa na madaktari kwa wagonjwa na hivyo kupunguza hatari za usambazaji wa virusi baina ya wagonjwa wa Covid-19 na wahudumu wa afya," alisema waziri huyo awali akihojiwa na Radio Rwanda.

"Pamoja na kuwapelekea wagonjwa dawa, roboti hizo pia zitatumika kupima viwango vya joto katika maeneo mengine ya umma kama vile vituo vya mabasi pamoja na kwenye milango ya kuingia katika maduka ya jumla ya bidhaa," alisema.

Tangu ulipotokea mlipuko wa COVID-19, Rwanda imekuwa ikitumia mfumo wa ndege ndogo zisio na rubani (drones) kuwasiliana na umma katika kuupa uelewa kuhusu ugonjwa huo. **BBC**



Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, akitoa maelezo zaidi ya kurejesha hali ya kawaida nchini humo, baada ya kuzindua sehemu ya kwanza ya mpango wa kuondoa marufuku ya kutotoka nje dhidi ya corona. **PICHA: MTANDAO**

# Kenyatta abadilisha viongozi wa chama Baraza la Seneti

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta (pichani), amebadilisha viongozi wa chama chake cha Jubilee katika baraza la seneti.

Aliyekuwa kiongozi wa wengi Kipchumba Murkomen na mnadhimu Susan Kihika wamevuliwa nyadhifa zao.

Kwenye taarifa kwa vyombo vya habari, Kenyatta alisema hatua hiyo inalenga kukiimarisha chama hicho, lakini wachambuzi walisema ulinuia kumvunja nguvu naibu wake, William Ruto.

Kikao hicho kilifanyika mapema asubuhi Ikulu ya Nairobi na kuhudhuriwa na maseneta 20 wa vyama vya Jubilee na KANU huku maseneta 19 wanaoegemea upande wa Makamu wa Rais wakikosa kuhudhuria.

Wakati wa mkutano huo, Mkuu wa Maseneta, Samuel Poghisio, seneta wa jimbo la Pokot Magharibi alichaguliwa kuwa kiongozi wa wengi katika Bunge la seneti.

Poghisio anachukua nafasi ya seneta Murkomen ambaye anaegemea upande



wa Makamu wa Rais, William Ruto. Inaaminika kuwa cheche zake dhidi ya Rais Kenyatta zilichangia kumuondoa kwenye wadhifa huo.

Siku chache zilizopita aliikosoa serikali ya Rais Kenyatta kwa kuweka uongozi wa kijeshi katika jimbo la Nairobi.

Seneta Irungu Kang'ata wa jimbo la Murang'a atakuwa mnadhimu wa walio wengi katika baraza hilo la Seneti. Anachukua nafasi ya seneta Susan Kihika ambaye amekuwa akiandamana na Makamu wa Rais, William Ruto kwenye mikutano ya hadhara ya kisiasa.


Seneta Fatuma Dullo wa jimbo la Isiolo anachukua wadhifa wa Naibu Kiongozi wa wengi katika baraza hilo la bunge.

Kimani Icungwa ni mbunge wa Jubilee na pia mwenyekiti wa kamati ya bajeti bungeni.

"Kama Rais wa Jamhuri ya Taifa la Kenya, anastahili kuangazia vitu vinavyomgusa mwananchi wa kawaida. Vitu anavyovifanya kwa sasa vinalenga kumnufaisha tajiri na kikundi cha wanasiasa, siyo kwa maslahi ya wakenya." Ichungwa alisema.

Ujio wa maseneta wa chama cha Kanu unajiri siku chache baada ya chama hicho kufanya mkataba wa ushirikiano na chama cha Jubilee.

Aidha, unaongeza nguvu ya idadi ya maseneta na wabunge wanaoegemea upande wa Rais kwenye mabaraza mawili ya Bunge. **DW**




# VAN DIJK BEKI BORA EPL-KOMPANY

**LIVERPOOL,** England

NYOTA wa Liverpool, Virgil van Dijk ni beki bora zaidi wa kati kwenye Ligi Kuu ya England, kwa mujibu wa Vincent Kompany.

Van Dijk mwenye umri wa miaka 28, ameng'ara tangu alipotoka Southampton na kutua Liverpool, kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 75, Januari mwaka 2018.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi alimaliza nafasi ya pili nyuma ya Lionel Messi kwenye tuzo za Ballon d'Or mwaka jana, akiwa ameisaidia Liverpool kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mkongwe wa Manchester City, Kompany, kwa sasa akiwa kocha mchezaji pale Anderlecht, anaamini Van Dijk ni beki bora wa kati kwenye historia ya Ligi Kuu ya England.

"Ninamchagua Virgil van Dijk," alisema akiiambia SPORF.

"Inashangaza, kwa sababu hajakuwa kwenye mchezo huo kwa muda mrefu, hasa ikizingatiwa kwamba kuna majina makubwa kama- John Terry na Rio Ferdinand, watu ambao wamecheza kwa muda mrefu.

"Lakini ishara zimeonyesha katika miaka yake michache, na kwamba angekuwa kwa muda mrefu angekuwa daraja la juu kabisa."

# Neymar, Mbappe hakuna wakuondoka PSG-Herrera

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR na Kylian Mbappe wamejitolea Paris Saint-Germain, hiyo ni kauli ya Ander Herrera wakati akimwagia maji ya baridi uvumi kuhusu uhamisho wao.

Nyota wa PSG, Neymar amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi kwa miamba wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Barcelona, ikiwa ni miaka mitatu tangu alipoondoka kwa ada iliyoweka rekodi ya euro milioni 222.

Huku Mbappe naye amekuwa akiripotiwa kuwaniwa na Real Madrid, ambao kocha wake, Zinedine Zidane hajaficha siri ya kuonyesha kuvutiwa naye.

Hata hivyo, mchezaji mwenzao wa PSG, Herrera, anaamini wawili hao wana furaha kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

"Mbappe na Neymar bado wapo PSG licha ya hali iliyopo sasa," alisema Herrera akinukuliwa na COPE.

"Nilikula chakula cha usiku na Neymar kabla ya karantini na alihusika katika kila mradi wa timu. Aliniambia hajawahi kukosa furaha jijini Paris.


"Mradi wa PSG ni kuhakikisha kwamba wote tunatimiziwa mahitaji yetu hapa Paris."

PSG walipewa ubingwa wa Ligue 1 baada ya msimu wa 2019-20 kufutwa mwezi uliopita kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Tangu alipoondoka Barca na kutua PSG mwaka 2017, Neymar ameshinda mataji matatu ya Ligue 1, Coupe de France, Coupe de la Ligue na Trophee.

Mbappe, ambaye awali alijiunga na PSG kwa mkopo kutoka Monaco mwaka 2017, amesherehekea mataji kama ya Neymar.






# Maguire akunwa na kipaji cha Rashford

**MANCHESTER,** England

NAHODHA wa Manchester United, Harry Maguire amemtaja Marcus Rashford kama mmoja wa wachezaji wenye kipaji cha juu zaidi kuwahi kucheza naye.

Rashford mwenye umri wa miaka 22, alikuwa akifurahia msimu wake bora, akifunga mabao 19 katika mechi 31, kabla ya kuumia mgongo Januari mwaka huu.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa England ameendelea kuimarika na Maguire amepaza sauti ya kusifia kipaji cha mchezaji mwenzake huyo wa United.

"Nafikiri kama klabu, unatakiwa kutumia nafasi yako ya unahodha vizuri, lakini kuongoza majukumu kwenye kundi," alisema mlinzi huyo akinukuliwa na UTD Podcast.

"Marcus yuko pale na anapambana katika kila mchezo. Bahati mbaya aliumia mgongo, lakini anapigana kurudi uwanjani. Kwa uhakika kabisa 'amemisi' sana kucheza soka.

"Mara zote anataka kuwapo mchezoni. Nafikiri unaweza kumuona mara kwa mara hata nje ya dimba, anaonyesha ubora wa kazi yake na anapambana sana, kitu ambacho ni kizuri kukishuhudia kwake.

"Dimbani kama nilivyosema, anavutia. Ni mmoja wa wachezaji bora zaidi ambaye nimewahi kucheza naye."

HABARI MICHEZO

# Thiago ataka kubaki PSG

**PARIS,** Ufaransa

THIAGO Silva angependa kukaribisha nafasi ya kuendelea kukaa na Paris Saint-Germain, kwa mujibu wa mke wa mlinzi huyo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu wa 2019-20 na pengine amecheza mechi yake ya mwisho ya Ligue 1 kwa klabu hiyo, baada ya msimu kufutwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Silva alihamia Ufaransa mwaka 2012 na ameshinda mataji saba ya ligi akiwa na PSG, ingawa ameshindwa kuisaidia klabu hiyo iliyotumia fedha nyingi kwenye usajili kupata mafanikio kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakiwa wanaishia robo fainali pekee.

Majaliwa ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 35 sasa yapo shakani na amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi katika klabu yake ya zamani ya AC Milan ya nchini Italia, lakini Isabelle Silva amebainisha kwamba mume wake anaweza kuongeza mkataba wa kubakia Paris.

"Thiago ana mahusiano mazuri na PSG na mashabiki wake," alisema akiliambia gazeti la Le Parisien.

"Hata kama mkataba wake utaendelea au la pale PSG, tutakuwa tunakwenda kuwaona marafiki zetu jijini Paris.

"Lakini kwa upande wetu, itakuwa vizuri zaidi kuendelea kubakia PSG, kwani tunaipenda klabu, jiji lao na nchi yote ya Ufaransa."





# WERNER ATAFITI LIVER - KOCHA

**MUNICH,** Ujerumani

NYOTA wa RB Leipzig, Timo Werner atafiti vizuri zaidi katika klabu ya Liverpool, kwa mujibu wa kocha wake wa zamani, Ralf Rangnick.

Werner mwenye umri wa miaka 24, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia kwa vinara hao wa Ligi Kuu ya England, baada ya kufunga mabao 27 kwenye mechi 36 za RB Leipzig msimu huu.

Rangnick, kocha wa zamani wa Leipzig ambaye kwa sasa ni mkuu wa maendeleo ya soka hapo Red Bull, anataka Werner abaki, lakini anahisi Liverpool kutamfaa zaidi mshambuliaji huyo.

"Ligi siyo muhimu sana, lakini kwa klabu naona kabisa pale panamfaa na anaweza kuwa na mafanikio makubwa zaidi akicheza Liverpool," alisema akiliambia gazeti la BILD.

"Tangu Timo alipoonyesha maendelezo mazuri chini ya Julian Nagelsmann, silaha yake kubwa ni kasi na nguvu awapo dimbani.

"Hivyo basi, atafiti zaidi kucheza katika Klabu kama Liverpool, ambayo inacheza kwa staili kama yake, lakini ningependa yeye abaki hapa."

Werner amefurahia misimu minne akiwa na RB Leipzig, akifunga mabao 88 katika mechi 150 kwa klabu hiyo tangu alipojiunga nayo akitokea Stuttgart mwaka 2016.

# *Lyon wahofia Depay kusepa*

**LYON,** Ufaransa

RAIS wa Klabu ya Lyon, Jean-Michel Aulas anahofia Memphis Depay anaweza kutafuta timu mpya baada ya maamuzi ya kufutwa kwa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, kwani nafasi waliyopo hawatafuzu kucheza mashindano ya Ulaya.

Kipindi kilichobaki cha msimu wa Ligi Kuu ya Ufaransa kilifutwa baada ya Waziri Mkuu, Edouard Philippe kuongeza muda wa kuzuia mikusanyiko na matukio ya michezo hadi Septemba mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Timu nyingi zilikuwa zimebakiwa na mechi 10, huku Lyon ikiachwa nafasi ya saba ambapo ilitarajia kwamba ingepambana ili kupata nafasi ya kufuzu kucheza mashindano ya Ulaya.

Lyon sasa wanaweza kufuzu kucheza mashindano hayo kama itashinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwani wanaongoza katika mchezo wa kwanza wa hatua ya 16-bora kwa ushindi wa 1-0 dhidi ya Juventus.

Lakini sasa majaliwa ya Depay, ambaye amekulia hapo Lyon yanaonekana kuwa shakani na Aulas ambaye anataka kumbakisha raia huyo wa Uholanzi anaona nafasi hiyo ni ndogo.

Akizungumza na Le Progres, alisema: "Nitafanya kila kitu kuhakikisha nawabakisha wachezaji wote.

"Lakini wachezaji wengine wanataka kucheza michuano ya Ulaya na wanaweza kwenda sehemu nyingine ili watimize ndoto zao.


"Sina habari yoyote kwa sasa. Memphis aliniambia kwamba yupo tayari kujadiliana kuhusu mkataba mpya mara atakaporudi.

"Wakala wake amesema anafikiria zaidi uwezekano wa kuondoka kama hatutafuzu kucheza mashindano ya Ulaya."



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# PIQUE: HATUONANI NA MESSI MAZOEZINI

## ●●● Napishana naye tu kwenye eneo la kuegesha magari na huwa...

**BARCELONA,** Hispania

GERARD Pique amesema hajamuona mchezaji mwenzake Lionel Messi akijifua kwenye mazoezi ya Barcelona wakati Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, ikijiandaa kurudi kwa wachezaji kujifua kivyao wakati huu wa mlipuko wa virusi vya corona.

**Messi na Barca walirudi kwenye mazoezi Ijumaa, wakiwa wamegawanywa kwenye viwanja vitatu tofauti ili kuwapo kwa wachezaji kujitenga na kutokaribiana.**

Barca waliendelea na mazoezi Jumamosi wakati kukiwa na matumaini LaLiga itarudi katikati ya Juni, baada ya kusimamishwa Machi mwaka huu.

"Sijawa na mawasiliano yoyote ya uwanjani na Messi, nimezungumza naye kwa njia ya simu mara nyingi," alisema Pique mlinzi wa Barca akinukuliwa na Movistar's El Partidazo.

"Sijamuona akijifua mazoezini, nimepishana naye tu kwenye sehemu ya kupaki magari mara nyingi. Wachezaji wote wanafanya mazoezi katika viwanja tofauti.

"Mimi nipo na Sergi Roberto na (Sergio) kwenye uwanja mmoja, lakini tumetengwa."

Barcelona ambao ni mabingwa watetezi walikuwa wanaongoza kwa pointi mbili kileleni dhidi ya wapizani wao Real Madrid baada ya kucheza mechi 27, kabla ya msimu kusimamishwa.Kocha mkuu wa Barca, Quique Setien awali alinukuliwa akisema kwamba, lingekuwa jambo la busara ubingwa wa ligi hiyo kupewa wao na msimu kusitishwa, huku golikipa wa Madrid, Thibaut Courtois akipinga jambo hilo.

Hata hivyo, Pique angependa msimu huo kumalizwa kwa mechi zilizobaki akiongeza: "Najua mpango wa LaLiga kumalizwa kwa kuchezwa, kwani inamaana kubwa, licha ya kwamba kuna hatari.

"Licha ya kuwa viongozi, ingekuwa vibaya kumaliza msimu kwa kuufuta.

"Tumetumia muda mwingi viwanjani na tunatakiwa kujiandaa kuepuka hatari zote za majeruhi, siku chache za mazoezi haitakuwa mbaya."

"Wamekuwa wakitupa taarifa mara kwa mara; (Rais wa LaLiga), Javier Tebas amejitolea muda wake mwingine," alisema Pique.

"Kuna watu ambao wanaogopa na ni muhimu kwamba kila mmoja afuate sheria kadri inavyowezekana. Ni vizuri kufanya mazoezi kama kundi, lakini kwa sasa tunatakiwa kuzoea kufanya kwa kujitenga."

## ZISIKUPITE

### SIRI AUBAMEYANG MADRID

MSHAMBULIAJI wa Arsenal na Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 30, alimuahidi marehemu babu yake kuwa atachezea Real Madrid. ***(Sun)***

### ARSENAL KUMKOSA DAYOT

KLABU ya Arsebal inakabiliwa na pigo la kumkosa beki wa RB Leipzig, Dayot Upamecano mwenye umri wa miaka 21 raia wa Ufaransa, baada ya wakala wake kusema kuwa huenda asihame kutokana na janga la virusi vya corona. ***(Sport 1)***

### SHANGHAI WASUBIRIA IGHALO

KLABU ya Shanghai Shenhua ya nchini China inatarajia kuwa mshambuliaji wake, Odion Ighalo mwenye umri wa miaka 30 raia wa Nigeria, atarejea klabuni hapo baada ya kuichezea Manchester United kwa mkopo, kabla ya msimu mpya wa Ligi Kuu ya China, ambao umepangwa kuanza Julai. ***(Sky Sports)***

### UTD YAJIPANGA KWA MARTINEZ

MANCHESTER United imefufua mpango wao wa kutaka kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan na Argentina, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 22. ***(Daily Mail)***

### SPURS, ARSENAL KWA WILLIAN

TOTTENHAM Hotspur na Arsenal zipo kwenye mbio moja ya kuwania kumsajili kiungo wa pembeni wa Mbrazil Willian kwa sababu majadiliano ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 31 kwa ajili ya kuongeza mkataba wake na Chelsea yamegonga mwamba. ***(football.london)***

### DORTMUND YATUA CHELSEA

BORUSSIA Dortmund wanataka kumsajili kinda wa Chelsea ambaye anacheza nafasi ya kiungo, Charlie Webster mwenye umri wa miaka 16 na kumpandisha hadhi hadi kiwango cha Jadon Sancho. ***(Sun)***

### LYON HOFU YATANDA

RAIS wa Lyon Jean-Michel Aulas, amekiri kwamba itakuwa vigumu kwa klabu hiyo kuwabakiza wachezaji wake nyota msimu huu - licha ya tetesi kuwa Chelsea inamnyatia mshambuliaji Ufaransa mwenye umri wa miaka 23, Moussa Dembele. ***(Star)***

### ARSENAL YAITIWA MBRAZIL

BABA mzazi wa kiungo wa kati wa Brazil, Gerson amedai kuwa Arsenal na Tottenham zinapania kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 kutoka klabu ya Flamengo. ***(ESPN)***

### LAMPARD ANUSA KITU NAPOLI

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard ametumia mtandao wa kijamii wa Instagram kumfuatilia Dries Mertens, na ripoti zinasema Lampard amewasiliana moja kwa moja na mashambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 33 raia wa Ubelgiji anayecheza pale Napoli. ***(Express)***

### CAMAVINGA BADO LULU REAL

REAL Madrid bado wanaangalia uwezekano wa kumsajili kinda wa Rennes ya Ufaransa, Eduardo Camavinga mwenye umri wa miaka 17, ambaye pia anawindwa na Manchester United. ***(AS)***

## HABARI MICHEZO



Kiungo wa Yanga, Mnyarwanda Haruna Niyonzima, akifanya mazoezi na wachezaji wa timu mbalimbali ufukweni mwa Bahari ya Hindi jijini Dar es Salaam juzi, kujiweka fiti kipindi hiki klabu yake ikiwa imesitisha mazoezi ya pamoja kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19). **NA MPIGAPICHA WETU**

# MWENGE YAOMBEA LIGI KUU Z'BAR IFUTWE

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HUKU ikionekana kuwa katika wakati mgumu wa kuweza kusalia Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao, Kocha Mkuu wa timu ya Mwenge, Salum Bajaka amesema ni vema ligi hiyo ikafutwa ili timu na wachezaji zianze kujipanga kwa ajili ya msimu mpya.

Kauli hiyo ya Bajaka inakuja wakati huu timu hiyo yenye makazi Kisiwani Pemba, ikiwa katika mstari wa hatari wa kushuka daraja kutokana na kushika nafasi ya 14 baada ya kuvuna alama 13 zilizotokana na mechi 19 kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 ambapo msimu huu jumla ya timu sita zitachuka daraja.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo alisema tangu kusimama kwa ligi hiyo na serikali kupiga marufuku mikusanyiko imekuwa vigumu kufanya mazoezi ya pamoja na wachezaji, hivyo endapo ligi hiyo itaendelea timu zitakosa nafasi ya kujipanga kufanya vizuri na hata kujinasua kushuka daraja.

**Alisema timu yao ya Mwenge inapendekeza ni vema msimu huu ukafutwa na kuanza msimu mpya ambao utatoa nafasi kwa timu kujipanga zaidi na kucheza ligi hiyo kwa ushindani ikilinganishwa na hivi sasa ambapo imesimama kwa muda mrefu tangu kutangazwa kwa janga la virusi vya corona hapa nchini, Machi 17, mwaka huu.**

"Timu zetu ni maskini hali zetu tunajuana, ni ngumu hata mchezaji kumudu vifaa vya kufanyia mazoezi, hivyo hata ligi ikiendelea baadhi ya timu kama yetu itakosa maandalizi ya haraka ya kujiandaa kwa ligi, kwa kuwa wachezaji wamekaa muda mrefu bila mazoezi ya pamoja," alisema.

Aidha, alisema endapo serikali itatoa tamko na mwongozo wa kuendelea kwa ligi hiyo, timu hiyo itacheza ligi na kuhakikisha inajinasua na janga la kushuka daraja japo katika mazingira magumu watakayokabiliana nayo.

Hata hivyo, Bodi ya Ligi na Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), wanasubiri muongozo kutoka serikalini juu ya ligi hiyo kurejea ama la.

# Gwambina FC yaanza mikakati Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inajiimarisha kuchumi kuelekea Ligi Kuu Bara, uongozi wa Gwambina FC umeanza mpango mkakati wa kuwakaribisha wadau wa soka kujitangaza kupitia klabu hiyo yenye makazi yake Misungi mkoani Mwanza.

Gwambina iliyopo Kundi B kwenye kinyang'anyiro cha Ligi Daraja la Kwanza, inahitaji alama sita tu katika michezo mitano iliyobaki kabla ya ligi hiyo kumalizika, ili kujihakikishia nafasi ya kupanda Ligi Kuu msimu ujao.

Katika msimamo wa kundi hilo lenye timu 12, Gwambina ipo kileleni ikiwa na alama 37 ikifuatiwa na Geita Gold FC yenye pointi 27 na Arusha FC ikishika nafasi ya tatu kwa alama zake 25, zote zikishuka dimbani mara 17.

Endapo ligi hiyo itarejea baada ya kusimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona, Gwambina ambayo ni miongoni mwa timu zilizoonyesha mwanga wa kupiga hatua kubwa kisoka nchini, ina asilimia kubwa ya kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

Na kutokana na matarajio hayo, Ofisa Masoko wa Gwambina FC, Mohamed Ngaiza amewaomba wadau kujitokeza kwa wingi kuwekeza ndani ya timu hiyo.

"Kuelekea msimu ujo, idara ya masoko tutakuwa na punguzo kubwa la matangazo, hivyo ni fursa kwa wafanyabiashara wote kuja kwa wingi kuwekeza katika klabu yetu.

"Klabu yetu ipo vizuri katika kutangaza bidhaa na matangazo ya wadhamini wetu kuanzia kwenye jezi na vifaa vyote vya michezo, hivyo ninawaomba wadau na wafanyabiashara wajitokeze kwa wingi," alisema.

Bodi ya Ligi nchini (TPLB), tayari imeeleza huenda ligi hiyo pamoja na Ligi Kuu na ile ya Daraja la Pili, zikarejea tena mapema Juni mwaka huu, endapo watapata baraka za serikali.

# Mpongo atoa darasa la usajili

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA kipa wa Coastal Union ya Tanga, Juma Mpongo amewakata wachezaji wazawa kuwa makini katika suala zima la vipengele vilivyopo kwenye mikataba wanayoingia kipindi cha usajili.

Mpongo ambaye amewahi kuitumikia KCB ya Kenya inayoshiriki Ligi Kuu nchi humo, ameliambia Nipashe kuwa kuelekea kipindi cha usajili wachezaji hususan wazawa, wanapaswa kuwa makini kwa kusoma na kuelewa vema mikataba yao kipengele kwa kipengele kabla ya kusaini.

Alisema mara nyingi wachezaji wazawa wamekuwa wanasaini mikataba bila ya kusoma vipengele vya mikataba hiyo zaidi ya kuangalia kiasi cha fedha za usajili na mshahara.

"Sasa hivi soka la Tanzania liko vizuri na kibiashara kuliko wakati tumeanza sisi, hivyo wachezaji wanatakiwa kuwa makini katika vipengele vya mikataba wanayoingia hasa kila kipengele kiwe kinabeba pande zote mbili.

"Ukiangalia katika mikataba wanayoingia wachezaji wazawa wanapoingia huwa kipengele cha endapo kuna timu kutoka nje itakapokuja basi klabu iwe rahisi kumruhusu, lakini pia wanatakiwa kuangalia zaidi maslahi yao katika mshahara kuliko ile ya kusaini," alisema Mpongo.

Alisema mikataba mingi ambayo wanaingia wachezaji wazawa waangalie vipengele vya kuwabeba siku wakiachwa au kupata timu nje ya nchi.

Mpongo alisema kutoka kwake nje ya nchi, amejifunza mambo mengi ikiwamo haki za mchezaji hasa kuingia mikataba na klabu husika.

Michezo
Jumanne Mei 12, 2020
Nipashe



Pique: Hatuonani na Messi mazoezini UKURASA 22

HAPA KAZI TU...



Kipa wa KMC FC, Juma Kaseja, akiwa mazoezini na beki wa timu ya wanawake ya Simba, Fatuma Issa 'Densa' (jezi namba 5) ufukweni mwa Bahari ya Hindi jijini Dar es Salaam, kipindi hiki klabu zao zikiwa zimesitisha mazoezi ya pamoja na kikosi, kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19). **NA MPIGAPICHA WETU**

# UKWELI MWAMNYETO USAJILI SIMBA, YANGA

## ●●● Mbio zaielemea Msimbazi, uongozi Coastal Union waanika zinapokwama ni...

**Na Saada Akida**

LICHA ya awali kuelezwa Simba imefikia hatua nzuri katika mpango wa kuipata huduma ya beki wa kati wa Coastal Union, Bakari Mwamnyeto, Yanga imeongeza kasi na kuizidi mbio za kumsajili nyota huyo aliyepo katika ubora wa hali ya juu kwa sasa, imeelezwa.

**Tangu kipindi cha dirisha dogo la usajili, Mwamnyeto amekuwa akihusishwa na klabu hizo kongwe nchini, na Simba ilidaiwa kumalizana na beki huyo na kudaiwa kwamba wamekubaliana amalizie msimu na timu yake hiyo.**

Hata hivyo, taarifa hizo sasa zinaonekana kuelea baada ya uongozi wa Coastal Union kuelezea jinsi mbio zinavyoendelea dhidi ya wakongwe hao wa soka nchini katika kuisaka saini ya beki huyo ambaye amekuwa nguzo kubwa kwa 'Wagosi Wakaya' hao msimu huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Coastal, Hemed Aurora alisema awali timu zote zilifika mezani na kuhitaji kufanya mazungumzo na kisha kuelezwa dau linalohitajika na timu hiyo.

Alisema katika usajili wa dirisha dogo walishindwana dau na Yanga, lakini Simba ilibisha hodi na kueleza dhamira yao ya kuhitaji huduma yake kwa msimu ujao.

"Baada ya Yanga kushindwa, tulikuwa tunawasikilizia Simba ambayo ilieleza kuwa inamhitaji kwa msimu ujao, ila hivi karibuni Yanga wameibuka tena na hawajakata tamaa kutaka mazungumzo zaidi kwa ajili ya kupata saini ya beki wetu.

"Kwa sasa Yanga wameanza tena kutaka [tuketi] kuzungumza, wamekuwa wakimfuatilia sana, na Simba kwa sasa wapo kimya baada ya kuwaeleza dau letu, hatujui dhamira yao ni nini na muda bado wa usajili," alisema Aurora.

Alisema kutokana na mahitaji ya nyota wao huyo ndani ya kikosi chao, wanahitaji kumuuza kwa dau ambalo litawawezesha kusajili nyota wengine kuziba pengo lake.

"Kwetu tunachoangalia ni nani atakuja kutimiza masharti tuliyowapa ikiwamo maslahi kwa pande zote, kama Yanga wakiweza sawa, lakini huu ukimya wa Simba bado hatujajua kama wamekata tamaa au wanajipanga vipi," alisema Aurora.

Mwamnyeto ameiongoza vema safu ya ulinzi ya Coastal Union msimu huu kwa kuiwezesha kuwa timu ya pili kuruhusu mabao machache (19) baada ya Simba iliyoruhusu nyavu zake kutingishwa mara 15 tu katika ligi hiyo yenye timu 20.

Pia Mwamnyeto ameisaidia Coastal Union kushika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 46 wakati huu Simba ikiwa kileleni na pointi 71 ikifuatiwa na Azam FC pointi 54, timu zote zikicheza mechi 28, huku Yanga iliyoshuka dimbani mara 27 ikifuata na alama zake 51 baada ya kuizidi Namungo FC kwa pointi moja.

# Miraji atamani ligi irejee Simba

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kushindwa kuitumikia klabu yake tangu mzunguko wa pili umeanza, winga mshambuliaji wa Simba, Miraji Athuman, amesema kwa sasa ana uchu mkali wa kurejea tena dimbani kutokana na kupona majeraha yake ya kifundo cha mguu yaliyokuwa yamemweka benchi.

Winga huyo aliyesajiliwa na Simba msimu huu akitokea Lipuli ya Iringa, hadi anapatwa na majeraha hayo, alishaifungia Simba mabao sita kati ya 63 ambayo wachezaji wenzake wamefunga hadi ligi hiyo inasimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona Machi 17, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Miraji alisema wakati akiwa nje kuuguza majeraha, kulikuwa kunamkosesha amani, lakini sasa amepona na anatamani ligi hiyo irejee tena mapema aitumikie klabu yake.

"Kwa sasa naendelea na mazoezi, nimepona, nashukuru na nimeruhusiwa kufanya mazoezi ya aina yote, nasubiri ligi tu irejee uwanjani," alisema nyota huyo. "Mazoezi nafanya nyumbani, ufukweni na gym, mimi ni mchezaji na hiyo ndio kazi yangu kubwa inayonifanya nimudu maisha, nasubiri kuona narejea tena uwanjani kuitumia timu yangu."

Nyota huyo kama walivyo wachezaji wengine wa Ligi Kuu, amekuwa akifanya mazoezi binafsi tangu ligi hiyo iliposimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona ambavyo hadi jana jioni jumla ya watu 4,215,274 duniani kote walishabainika kupata maambukizo huku kati yao waliopona wakiwa ni 1,506,231 na vifo 284,672.

Kwa Tanzania pekee hadi jana bado idadi ya walioambukizwa ilikuwa 509 na waliopona wakiwa 183, huku waliopoteza maisha kutokana na virusi hivyo vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19 wakiwa ni 21.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >